

**CHANGAMOTO ZA KUTUMIA ISTILAH MBILI KWA DHANA MOJA  
KATIKA KUFUNDISHA ISIMU NA FASIHI SHULE ZA SEKONDARI:  
MIFANO KUTOKA MKOA WA KUSINI - PEMBA, TANZANIA**

**SALEH ALI ABDALLA**


**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA  
KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU**

**HURIA TANZANIA**

**2016**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii yenye mada: *Changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari: Mfano kutoka mkoa wa Kusini Pemba, Tanzania*, na anapendekeza kwamba inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ikiwa ni sehemu ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya M.A (Kiswahili) katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.



.....

**Prof. James S. Mdee**

**(Msimamizi)**

10-10-2016

.....

Tarehe

**HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuiga, kutolewa kivuli au kuchapishwa upya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### **TAMKO LA MTAHINIWA**

Mimi, **Saleh Ali Abdalla**, natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo “*Changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari: Mfano kutoka mkoa wa Kusini Pemba, Tanzania* ” ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitowasilishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada kama hii.

.....  
Saini

.....  
Tarehe

**TABARUKU**

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu Bibi Fatma Sharif Bakar na Bwana Ali Abdalla, kwa malezi na mapenzi yao yaliyonisaidia katika nyanja mbalimbali za maisha yangu. Pia kwa mke wangu na familia yangu yote. Ninamuomba Mungu aendelee kuyabariki maisha yao.

AMINA

## SHUKURANI

Awali sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu, uzima, uwezo na afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu hadi kukamilika kwa kazi hii. Kazi ya utafiti ni kazi nzito, inahitaji ushirikiano, utulivu, uvumilivu, maoni na miongozo mbalimbali kutoka kwa msimamizi. Shukrani za dhati na za pekee kabisa ni kwa mwalimu wangu, mlezi wangu na msimamzi wangu, Prof. James Salehe Mdee, kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Ufaavu wake kwangu hauwezi kukisiwa, kupigiwa mfano wala kulipwa. Kwangu ni kumuomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ili na wengine waweze kupata lulu ya taaluma aliyonayo mtaalamu huyu. Pia ninatoa shukrani za dhati kwa wazazi wangu: Mzee Ali Abdalla Mjemba na Bibi Fatma Sharifu Bakari, kwa uvumilivu wao hasa nilivyowasumbua wakati wa kukua kwangu. Kama sio uvumilivu wao nisingeweza kufika hapa na hivyo kazi hii isingewezekana. Mungu awazidishie maisha mema yenye kheri ndani yake. Shukrani pia ziwaendee wahadhiri wangu wakiongozwa na Dkt Hanna Simpasa, Prof. E. Mbogo, Dkt. Lipembe, Dkt. Zelda Elisifa na Mwalimu Bakari Kombo. Vilevile natoa shukurani zangu za dhati kwa walimu wenzangu wote tuliofanya digrii hii pamoja kwa kunipa ushauri na kunielekeza pamoja na kunipatia vitabu mbali mbali vya marejeo.

**IKISIRI**

Utafiti huu umeshughulikia changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari za Tanzania. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili kwa shule za sekondari, kudadisi usuli wake na kupendekeza njia za kuondokana na tatizo hili. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo na mbinu ya usampulishaji iliyotumika ni usampulishaji nasibu tabakishi na umefanywa katika baadhi ya shule za mkoa wa kusini Pemba. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni mbinu ya dodoso. Kuhusu matokeo ya utafiti imebainika kwamba kuna matumizi makubwa ya istilahi mbili kwa dhana katika shule za sekondari katika kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili. Hali hii imesababisha wanafunzi kukanganyikiwa, kufeli na hata kulichukia somo. Kwa hivyo matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja ni dhahiri kuwa huathiri ujifunzaji wa isimu na fasihi ya Kiswahili. Mapendekezo yanayotokana na utafiti huu ni pamoja na kuanzisha vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi kwa ujumla.

## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO.....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TAMKO LA MTAHINIWA .....</b>	<b>iv</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>v</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>vi</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vii</b>
<b>ORODHA YA MAJEDWALI.....</b>	<b>xii</b>
<b>ORODHA YA NA VIELELEZO.....</b>	<b>xiii</b>
<b>ISTILAHI ZILIZOTUMIKA .....</b>	<b>xiv</b>
<b>ORODHA YA VIFUPISHO .....</b>	<b>xv</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>1.0 UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi wa Jumla .....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .....	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	4
1.4 Malengo ya Utafiti.....	5
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti.....	5
1.4.2 Malengo Mahsusi.....	5
1.5 Maswali ya Utafiti .....	5
1.6 Umuhimu wa Utafiti .....	6
1.7 Hitimisho .....	7



<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>8</b>
<b>2.0 MAPITIO YA TAFITI TANGULIZI NA NADHARIA</b>	
<b>ZILIZOTUMIKA .....</b>	<b>8</b>
2.1 Utangulizi .....	8
2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi .....	8
2.3 Nadharia ya Istilahi Kama Kiunzi cha Kinadharia cha Utafiti huu .....	10
2.3.1 Maana ya Nadharia .....	10
2.3.2 Nadharia ya Jumla ya Istilahi .....	11
2.3.3 Nadharia ya Istilahi na Dhana.....	12
2.4 Pengo la Utafiti .....	13
2.5 Hitimisho .....	14
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>15</b>
<b>1.0 USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>15</b>
1.1 Utangulizi .....	15
1.2 Usanifu wa Utafiti.....	15
1.3 Eneo la Utafiti.....	19
1.3.1 Walengwa wa Utafiti .....	19
1.3.2 Sampuli na Usampulishaji .....	20
1.4 Ukusanyaji wa Data.....	21
1.4.1 Aina za Data Iliyokusanywa.....	22
1.4.2 Mbinu za Kukusanyia Data .....	23
1.4.3 Zana za Kukusanyia Data .....	24
1.5 Uchambuzi wa Data.....	25
1.6 Hitimisho .....	25

<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>26</b>
<b>4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO .....</b>	<b>26</b>
4.1 Utangulizi .....	26
4.2 Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja.....	27
4.3 Matumizi ya Istilahi Mbili kwa Dhana Moja .....	30
4.4 Istilahi Mbili Zinazowakilisha Dhana Moja .....	32
4.5 Ufahamu wa Uwepo wa Istilahi zaidi ya Moja kwa Dhana Moja.....	34
4.6 Sababu za Kuundwa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja.....	36
4.7 Athari za Kutumia Istilahi Mbili katika Kuwakilisha Dhana Moja.....	39
4.7.1 Kuwakanganya Wanafunzi.....	39
4.7.2 Kushindwa Katika Mtihani kwa Wanafunzi.....	41
4.7.3 Wanafunzi Kulichukia Somo.....	42
4.7.4 Athari za Ujumla za Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja .....	43
4.8 Mambo ya Kufanya ili Kuepuka Matumizi ya Istilahi Tofauti kwa Dhana Moja.....	44
4.9 Hitimisho .....	47
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>49</b>
<b>5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>49</b>
5.1 Utangulizi .....	49
5.2 Muhtasari wa Utafiti .....	49
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	50
5.4 Mapendekezo kwa ajili ya Utafiti zaidi .....	51
5.5 Hitimisho .....	52

<b>MAREJELEO .....</b>	<b>54</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>58</b>

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.4.1: Ufahamu wa Kuwapo kwa Istilahi Mbili Zinazowakilisha Dhana Moja .....	29
Jedwali Na.4.2: Kiwango cha Utumiaji wa Istilahi Mbili Kuwakilisha Dhana Moja.....	31
Jedwali Na. 4.3: Ufahamu wa Seti ya Istilahi Mbili Zenye Kuwakilisha Dhana Moja.....	33
Jedwali Na. 4.4: Ufahamu wa Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja .....	35
Jedwali Na. 4.5: Mambo yaliyosababisha Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja.....	37
Jedwali Na. 4.6: Athari ya Kuwakanganya Wanafunzi .....	40
Jedwali Na. 4.7: Athari ya Kushindwa katika Mtihani kwa Wanafunzi .....	41
Jedwali Na. 4.8: Athari ya Wanafunzi Kulichukia Somo.....	42
Jedwali Na. 4.9: Athari za Ujumla za Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja ..	44

**ORODHA YA VIELELEZO**

Kielelezo Na. 4.1: Istilahi Mbili za Isimu Zenye Kuwakilisha Dhana Moja .....	27
Kielelezo Na. 4.2: Istilahi Mbili za Fasihi zenye Kuwakilisha Dhana Moja .....	28
Kielelezo Na. 4.3: Mfano wa Seti za Istilahi Mbili zenye Kuwakilisha Dhana Moja.....	32
Kielelezo Na. 4.4: Mchango wa Waandishi Katika Kuunda Istilahi Tofauti kwa Dhana Moja .....	38

## **ISTILAHI ZILIZOTUMIKA**

**Sampuli:** ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake.

**Usampulishaji:** ni utaratibu wa kuchagua washiriki mahususi kutoka katika kaumu ya watu au fungu la vitu ili washiriki hao waweze kuwa wakilishi wa watafitiwa katika eneo la utafiti watu hao (au vitu hivyo).

**Usampulishaji nasibu pangilifu:** ni njia ambayo watoa taarifa hugawanywa katika makundi na sampuli huchukuliwa kutoka katika kila kundi ili kupata data itakayoakisi kundi la watu wote wa eneo la utafiti.

**Mbinu ya masimulizi:** ni mbinu ambayo humtaka mtafiti kuangalia jambo kwa umakini na kulieleza kwa usahihi.

**Mbinu ya utafiti stahilifu:** ni njia ya kuchanganua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu.

**Usanifu wa utafiti:** ni utaratibu wa kuchunguza tatizo kisayansi.

**ORODHA YA VIFUPISHO**

BAKITA	- Baraza la Kiswahili Tanzania
BAKIZA	- Baraza la Kiswahili Zanzibar
J	- Jumla
KN	- Kirai nomino
KT	- Kirai tenzi
Na	- Nambari
NI	- Nadharia ya istilahi
NJI	- Nadharia Jumuishi ya Istilahi
TATAKI	- Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi wa Jumla**

Utafiti huu umechunguza changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari za Tanzania, hususan mkoa wa Kusini Pemba, katika wilaya za Mkoani na Chakechake. Katika sura hii tumeeleza vipengele muhimu vinavyohusu utafiti kwa ujumla ambavyo maelezo yake yamekitwa katika utafiti huu. Kipengele cha kwanza kinaeleza usuli wa tatizo ambapo tumeeleza kwa kifupi chimbuko la tatizo linalolengwa katika utafiti huu. Tamko kuhusu tatizo la utafiti limefuata na kisha malengo ya utafiti. Maswali ya utafiti ambayo yametafutiwa majibu katika utafiti huu. Hatimaye tumeeleza umuhimu wa utafiti na hitimisho la sura hii.

#### **1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Lugha ni chombo muhimu kwa ajili ya mawasiliano ya mwanadamu. Lugha huwawezesha wanalugha kupashana habari zinazohusu shughuli zao za kila siku na pia hutumiwa kutolea maarifa anuwai. Ili mawasiliano baina ya msemaji na msikilizaji yakamilike, ni lazima wahusika hao watumie ishara au msamiati ambao kila mmoja anauelewa. Hali hii hutokea katika lugha zote na hata vilugha vya lugha moja, iwe lahaja, rejesta au simo. Inapotokea kuwa msemaji hutumia msamiati usiojulikana kwa msikilizaji, mawasiliano hukatika. Lugha ya ishara, halikadhalika huweza kukamilisha mawasiliano baina ya msemaji na mtazamaji iwapo wote hutumia alama au ishara ambazo huibua maana ileile kwa kila mmoja.



Hali hii hutokea pia katika lugha ya kufundishia. Lugha ya kufundishia ni lugha iliyoteuliwa rasmi kutolea elimu. Tanzania imeteua Kiswahili na Kiingereza kuwa lugha za kufundishia. Lugha ya kufundishia haina budi kueleza dhana kwa uwazi na usahihi bila utata wowote. Ufundishaji wa masomo k.v. hisabati, fizikia, sayansi, fasihi na isimu unahitajii matumizi sahihi ya lugha ya somo ambayo ni msamiati mahsusi kwa somo hilo, yaani istilahi. Kwa hivyo, mwalimu wa somo au mwandishi wa kitabu katika somo husika hana budi kutumia istilahi zenye kueleza dhana hizo kwa uwazi na usahihi bila kuacha tashwishi yoyote kwa msikilizaji au msomaji.

Kiswahili ni lugha ya kufundishia masomo yote katika shule za msingi na katika shule za sekondari hufundishia somo la Kiswahili, hususan isimu na fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Massamba (2011) isimu ni taaluma ya sayansi ya lugha inayoshughulika na nadharia, uchunguzi na uchambuzi wa vipengele mbalimbali vya lugha kwa kutumia mbinu za kisayansi. Aidha Richards na wenzake (1985) wanasema kuwa isimu ni mtalaa ambao huchunguza lugha kama mfumo wa mawasiliano ya wanadamu. Kwa upande wa fasihi tumeelezwa na Wamitila (2003:13) kuwa fasihi ni sanaa itumiayo lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake. Fasili zote hizi za isimu na fasihi zinaonyesha kuwa hizi ni taaluma ambazo huelezeka kwa lugha mahsusi ambazo ni maalum kwa kila moja. Kwa kuwa masomo ya fasihi na isimu katika sekondari yana dhana za kisayansi, matumizi ya Kiswahili katika kufundishia yanamtaka mwalimu au mwandishi wa vitabu vya masomo hayo kutumia msamiati utakaoeleza dhana hizo bila kuacha shaka yoyote. Kinyume chake, dhana za somo husika hazitaeleweka kwa wanafunzi au wasomaji wa vitabu hivyo. Kwa kuwa isimu na fasihi ni taaluma za

kisayansi, utafiti huu ulitalii ufundishaji wa isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari tu.

Ufundishaji wa isimu na fasihi ya Kiswahili katika sekondari ambayo hufundishwa kwa Kiswahili unakabiliwa na changamoto ya lugha inayotumiwa kufundishia au kuandikia vitabu kwa fani hizi. Vitabu vya waandishi tofauti vinavyohusu mada moja hutumia istilahi mbili kueleza dhana moja, kwa mfano, Massamba na wenzake (1999) huigawa sentensi katika virai vikuu viwili: Kirai nomino (KN) na Kirai tenzi (KT), lakini Njogu na wenzake (2006) wanaigawa sentensi katika virai vikuu viwili ila hutumia istilahi tofauti: Kirai nomino (RN) badala ya KN na Kirai tenzi (RT) badala ya KT. Habwe na Karanja (2004:50) wakizungumzia juu ya aina za konsonanti, wanaeleza kuwa kuna konsonanti zinazoitwa vikwaruzo mfano [f, v, ð, z, h] lakini Mgullu (1999: 40) huziita konsonanti hizi kuwa ni vikwamizwa mfano [f], [v].

Katika kuainisha njia mbalimbali za uchanganuzi wa sentensi Nchimbi (2008) anataja uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya mishale lakini Nyangwine (2010) anaeleza njia hiyo hiyo ya uchanganuzi kuwa ni uchanganuzi kwa njia ya mistari. Besha (1994) katika kuzielezea fonimu za lugha anasema kuna aina ya fonimu iitwayo irabu, lakini Habwe na Karanja (2004) wanaeleza dhana hii kwa kutumia istilahi ya vokali.

Njogu na Chimerah (1999) katika kuzungumzia aina za wahusika, wanaeleza kuwa kuna wahusika bapa, lakini Semzaba (2006) anawaita wahusika wasiobadilika.

Mulokozi (1996) akizungumzia sanaa za maonyesho, huzungumzia aina ya sanaa ya maonyesho iitwayo drama, lakini Wamitila (2003) anaiita aina hii ya sanaa ya maonyesho kuwa ni maigizo.

Ameir na wenzake (1982) wanataja aina mojawapo ya tamthiliya kuwa ni vichekesho, lakini Wamitila (2002) anaelezea aina hii ya tamthiliya kwa kutumia istilahi ya futuhi.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Kwa kuwa lengo la kusoma ni kupata maarifa, msomaji ataelewa anachosoma iwapo kila dhana itaelezwa kwa neno moja ambalo ndio istilahi yake. Vitabu vilivyotungwa na wandishi tofauti wenye kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja huwakanganya wasomaji wao. Aidha, mwanafunzi naye ataelimika iwapo walimu wake watatumia istilahi moja kueleza dhana moja. Iwapo walimu tofauti wataifundisha mada moja kwa kutumia vitabu tofauti vyenye istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana moja, huu huwa ni mwanzo wa kuwakanganya wanafunzi.

Pia kama ilivyoonyeshwa hapo juu, kwamba hali hii huwafanya wanafunzi wasifanye vyema katika mitihani yao. Wanafunzi wakijibu kwa kutumia istilahi walizofunzwa na mwalimu wao au kujisomea vitabu lakini watahini wakawa na majibu yenye istilahi za waandishi wengine, athari yake ni kubwa kwa wanafunzi. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kuwa matumizi ya istilahi mbili katika kufundisha ni tatizo ambalo linahitaji kuchunguzwa, kujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi.

## **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahsusi manne.

### **1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili kwa shule za sekondari, kudadisi usuli wake na kupendekeza njia za kuondokana na tatizo hili.

### **1.4.2 Malengo Mahsusi**

Ili kufikia lengo kuu, utafiti huu umeshughulikia malengo mahsusi yafuatayo:-

- i) Kubaini uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja katika isimu na fasihi
- ii) Kueleza sababu za kuundwa istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundishia isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari.
- iii) Kubaini athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja kwa wanafunzi na jamii kwa jumla.
- iv) Kueleza jinsi ya kukabiliana na changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari.

## **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu una swali kuu moja la utafiti na maswali mahsusi sita. Swali kuu la utafiti linachanganuliwa katika maswali mahsusi.

### **1.5.1 Swali Kuu la Utafiti**

Kwa nini baadhi ya dhana za isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari zina istilahi mbili zinazoziwakilisha?

### **1.5.2 Maswali Mahsusi ya Utafiti**

- i) Je isimu na fasihi ya Kiswahili zina istilahi mbili au zaidi zinazotumika kuwakilisha dhana moja?
- ii) Ni mambo gani yalisababisha kuzuka kwa istilahi mbili zinazowakilisha dhana moja?
- iii) Kuna athari gani za kutumia istilahi zaidi ya moja katika kuwakilisha dhana moja?
- iv) Tunawezaje kuepuka au kuondokana na tatizo hili?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja yana athari kubwa kwa wanafunzi, kwani huweza kuwafanya wasifanye mithani yao kwa ufanisi. Hali hii huweza kutokea iwapo istilahi ambazo walimu wao wanazitumia zinatofautiana na istilahi zinazotumiwa na watahini kwa dhana ile ile. Mwanafunzi anayekabiliwa na hali hii anapofanya mtihani hushindwa kubaini kuwa dhana zinazoelezwa na istilahi za mtahini ni zile alizofundishwa japo kwa istilahi tofauti.

Kwa hali hii utafiti huu ni muhimu sana kufanyika ili kufahamu ukubwa wa tatizo, mambo yanayosababisha uwepo wa tatizo hili na namna ya kukabiliana na tatizo hili na kuliondoa kabisa.

Utafiti huu una umuhimu mkubwa kwa wadau mbalimbali wa isimu na fasihi ya Kiswahili kwani utawasaidia katika mambo yafuatayo

- (a) Walimu watabaini changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari.

- (b) Waandishi wa isimu na fasihi ya Kiswahili watatambua umuhimu wa kutumia istilahi moja kwa dhana moja.
- (c) Asasi zinazoendeleza Kiswahili Afrika Mashariki zitatambua haja ya kushirikiana katika kusanifisha istilahi za fani moja badala ya kila asasi ya nchi au wandishi wao kutunga na kutumia istilahi zao na kuweza kuzisanifisha istilahi hizo ili ziweze kutumika katika ufundishaji, ujifunzaji na utahini.
- (d) Watahini watahakikisha kuwa vitabu vinavyotumiwa kufundishia isimu na fasihi vina istilahi zilizosanifishwa ili nao wanapotunga mitihani watumie istilahi hizohizo ili kuepuka kuwakakanganya watahiniwa.
- (e) Utafiti huu utawasaidia wasomi na watafiti wengine wa lugha ya Kiswahili kuweza kugundua na kubaini changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja na kuchagua msamiati ambao ni muafaka kwa kila dhana.

## **1.7 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangalia usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali yaliyotuongoza katika utafiti wetu, pengo la utafiti kisha tumeonyesha umuhimu wa utafiti wetu kwa wadau mbalimbali wa Kiswahili na hususan istilahi za isimu na fasihi ya Kiswahili. Mapitio ya kazi tangulizi pamoja na nadharia ya utafiti huu zitazungumziwa katika sura inayofuata.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA TAFITI TANGULIZI NA NADHARIA ZILIZOTUMIKA**

#### **2.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumepitia baadhi ya kazi zilizofanywa na wataalamu mbalimbali juu ya changamoto za kutumia istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja. Aidha tumefafanua kiunzi cha nadharia kilichozingatiwa katika utafiti huu. Cozby na Bates (2012) wanaeleza kuwa mapitio ya maandiko ya kazi tangulizi zinazohusiana na utafiti unaokusudiwa kufanywa ni mchakato unaohusu uchunguzi wa kina wa maandiko yaliyotangulia katika eneo fulani la taaluma. Kazi hizo zinaweza kuwa zimechapwa katika vitabu, makala au majarida. Lengo hasa la kufanya mapitio lilikuwa kuchambua tafiti zilizofanyika ili kubaini pengo lililopo au kujua ni kwa kiasi gani mada ya utafiti ilikuwa imetafitiwa ili kuepuka kurudia mambo yaliyokwisha kufanywa. Mapitio ya kazi tangulizi humpa pia mtafiti fursa ya kubaini eneo ambalo halijachunguzwa ili kuliziba pengo hilo. Mapitio ya kazi mbalimbali hutoa mwongozo unaofaa kwa mtafiti. Mchakato mzima wa upitiaji wa kazi mbalimbali hufungamana na kanuni zake kama kuhakiki, kujadili na kutoa maoni ya mtafiti ili kuboresha utafiti unaokusudiwa kufanywa.

#### **2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi**

Buliba (1998) akizungumzia matatizo yanayokabili somo la isimu kwa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya, anaeleza kuwa walimu katika vyuo vikuu hutumia istilahi tofauti katika kuelezea dhana moja kwa mfano vokali/irabu, sauti/fonimu. Wengi waistilahi na vitabu vinavyoshughulikia isimu hutumia istilahi

zinazokanganya. Mfano taaswira/picha, mchoro/kielelezo tungo, kirai/kikundi. Hata hivyo, hakueleza sababu za uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja wala kuonyesha utatuzi wa changamoto alizoziona katika ufundishaji wa isimu katika vyuo vikuu.

Abass (2011) akizungumzia juu ya uchunguzi wa mambo yanayosababisha wanafunzi wa somo la Kiswahili kutolimudu vyema katika vyuo vikuu, anasema kwamba baadhi ya walimu hutumia istilahi tofauti katika kuelezea dhana moja kwa mfano: kirai/kikundi/kifungu. Hali hii husababisha wanafunzi wanapojifunza kuwa kikwazo kwao katika kuelewa istilahi iliyo sahihi. Licha ya mtafiti huyu kuelezea mambo yanayosababisha wanafunzi wa somo la Kiswahili kutolimudu vyema, lakini hakuzungumzia njia za kutatua tatizo hilo.

Omar (2012) akizungumzia matatizo ya kufundisha vyuo vya amali Zanzibar, alitaja ukosefu wa vitabu vya marejeo pamoja na walimu kutumia istilahi tofauti katika kuelezea dhana moja. Kwa mfano upeo/mawanda, migogoro/migongano, kiangaza mbele/viona mbele. Katika kulizungumzia hili, alieleza kuwa ni vyema kuwepo kwa asasi maalum Zanzibar inayoshughulikia matumizi ya istilahi. Suluhisho hili hapana shaka halikidhi haja, kwani Zanzibar peke yake haiwezi kutatua tatizo hili ikizingatiwa kuwa isimu na fasihi hufundishwa katika vyuo vikuu vya Tanzania na Kenya na vitabu vya masomo haya huchapishwa huko pia.

Sultan (1976) akizungumzia juu ya matatizo yanayokabili somo la isimu kwa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya, anasema kuwa mafunzo mengi yanayohusika na sayansi ya lugha ni magumu, hasa pale yanapofunzwa na walimu



wanaosema kuwa Kiswahili ni lugha ngumu isiyofahamika, pia anaelezea changamoto ya matumizi ya tofauti ya istilahi kwa dhana. Mathalani mifaanyiko/michakato, kiwakilishi/kibadala, pronomino/pronauni, muundo/umbo ambapo matumizi haya ya istilahi tofauti kwa dhana yanachafua lugha na kuwaathiri wanafunzi wengi. Hata hivyo, hakueleza sababu za uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja wala kuonyesha utatuzi wa changamoto alizoziona katika ufundishaji wa isimu katika vyuo vikuu.

Salim (2008), akizungumzia juu ya ugumu wa kufundisha fasihi kwa lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu, anasema kuwa walimu hutumia istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana ambazo ni kikwazo kwa wanafunzi kuweza kujifunza kwa urahisi. Matumizi haya ya istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana na uchache wa vitabu vinavyoshughulikia fasihi husababisha kutofanya vizuri katika kozi ya fasihi na husababisha kushuka kwa ufaulu wao.

Licha ya mtafiti huyu kutaja ugumu wa kufundisha fasihi katika vyuo, lakini hakuzungumzia juu ya sababu na utatuzi wa kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari.

## **2.3 Nadharia ya Istilahi Kama Kiunzi cha Kinadharia cha Utafiti huu**

### **2.3.1 Maana ya Nadharia**

Nadharia kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981) ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Hudson (1985) kama alivyonukuliwa katika Mekacha (2000) anaeleza nadharia kuwa ni

mahitimisho yanayotokana na uchambuzi wa data ambao hujaribiwa na ubora wake ukithibitika hutumiwa kama mwongozo wa utafiti. Nadharia huundwa kutokana na uchambuzi na ufafanuzi wa data za kitakwimu au data stahilifu na kuzifanyia majumuisho na kisha mahitimisho ya kinadharia (Mekacha 2000). Baada ya kuona maana ya nadharia sasa tuelezee nadharia za kiuchambuzi zilizokuwa viunzi vya utafiti huu. Utafiti huu umezingatia nadharia ya jumla ya istilahi kama ilivyoasisiwa na Wuester (1930) na nadharia ya istilahi na dhana ya McIntosh (1991).

### **2.3.2 Nadharia ya Jumla ya Istilahi**

Nadhariaya jumla ya istilahi ni nadharia inayoelezea asili ya dhana, msingi wa uundaji wa istilahi na umuhimu wa dhana kuwakilishwa na istilahi moja (Wuester 1930). Lengo kuu la nadharia hii ni kuzitofautisha istilahi. Kiunzi hiki cha kinadharia kinachunguza na kuchanganua matumizi ya istilahi katika kuwakilisha dhana.

Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu wa kiasustralia Wuster mnamo mwaka 1930. Kabala ya kuanzishwa kwa nadharia hii masuala ya istilahi yalikuwa yanasimamiwa zaidi na wanasayansi. Mnano karne ya 20 ilionekana kuwa istilahi haihusiki tu na kuvipa vitu majina bali kunahitajika makubaliano ya wadau wanaotumia istilahi hizo, ndipo wakandarasi na mafundi wakashirikishwa katika zoezi la utoaji wa istilahi. Hivyo uundaji wa istilahi ulihitaji kundi maalum la wataalamu.

Kufikia nusu ya karne ya 20 wanaisimu na wanaisimu jamii walianza kumakinikia masuala ya istilahi. Nadharia ya jumla ya istilahi ilipata kufahamika rasmi pale

mwanaisimu wuster alipoindika katika tasnifu yake ya shahada ya udaktari (PhD) mwaka 1930. Hivyo wuster katika kazi yake amesema kazi ya istilahi huanza na dhana na hufanya kazi katika dhana kwenda istilahi. Pia kuna wataalamu kadhaa ambao wanatambulika juu ya nadharia hii kama vile Alfred Scholmann wa Ujerumani, Ferdinand de Saussure wa Uswizi, E. Dresen wa Urusi na J. E. Holstrom kutoka uingereza ambapo wataalamu hawa wameitumia nadharia hii katika kuzitofautisha istilahi.

Wuester (ameshatajwa) anaeleza kwamba kuna uhusiano kati ya dhana na istilahi na kwamba nadharia ya jumla ya istilahi ina malengo yafuatayo

- a) Kuondoa utata katika lugha kwa njia ya kusanifisha istilahi ili kuzifanya kuwa njia bora ya mawasiliano.
- b) Kuwafahamisha wanazuoni umuhimu wa kutumia istilahi zilizosanifiwa wanaposhughulika na masuala ya kitaaluma.
- c) Kufanya istilahi kuwa ni somo (fani) kwa malengo ya kiutendaji.

Hivyo mtafiti ameitumia nadharia hii katika kuonyesha na kuondoa changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari kwa sababu ya umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja ambao huondoa utata na kufanikisha mawasiliano.

### **2.3.3 Nadharia ya Istilahi na Dhana**

Nadharia ya istilahi na dhana ni nadharia inayofungamanisha na kuunganisha dhana na neno linaloliwakilisha. Nadharia hii ambayo iliasisiwa na McIntosh (1991) inaeleza kwamba istilahi ni dhana ya kisayansi na kwamba haina budi kueleza dhana

kwa uwazi na usahihi bila ya kuwa na utata. Kiunzi hiki cha kinadharia kinazingatia umuhimu wa kutumia istilahi moja kwa dhana. Kupitia kiunzi hiki, wanaisimu huzichunguza lugha kwa kuangalia istilahi ili kuonyesha na kuelezea jinsi istilahi hiyo inavyowakilisha dhana. Pia kuna wataalamu kadhaa ambao wanatambulika juu ya nadharia hii kama vile Wiegleb, Loehle, McCoy, Shrader –Frechette ambapo wataalamu hawa wameitumia nadharia hii katika kuelezea istilahi moja katika kuwakilisha dhana moja.

Nadharia ya istilahi na dhana ina malengo yafuatayo

- a) Kueleza dhana kwa uwazi na usahihi bila ya kuwa na utata katika lugha kwa njia ya kusanifisha istilahi ili kuzifanya kuwa njia bora katika matumizi ya lugha.
- b) Kuifungamanisha dhana na neno linaloliwakilisha.
- c) Kutumia istilahi moja kwa dhana moja katika taaluma.
- d) Kuichunguza lugha kwa kuziangalia istilahi na kuweza kuonyesha istilahi hiyo inavyowakilisha dhana.

Hivyo mtafiti ameitumia nadharia hii katika kuonyesha na kuondoa changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari kwa sababu ya umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja ambao huondoa utata na kufanikisha mawasiliano kwa kueleza dhana dhana kwa uwazi.

## **2.4 Pengo la Utafiti**

Utafiti huu uliziba pengo la kitaaluma ambalo bado halijashughulikiwa na wataalamu wengi. Wataalamu walio wengi wanatazama changamoto za matumizi ya istilahi

tofauti kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari kwa kuelezea utumiaji wa istilahi tofauti kwa dhana moja na kutaja athari za utumiaji wa istilahi hizo, bila ya kuelezea sababu zilizochangia kuwepo kwa tatizo hili na namna ya kuliepuka hali hiyo. Kwa hivyo basi, katika utafiti huu tumeeleza mambo tofauti yaliyosababisha kuundwa kwa istilahi tofauti kwa dhana moja katika isimu na fasihi ya Kiswahili na kisha kutoa mapendekezo ya kuzingatiwa ili kuepukana na tatizo hili.

## **2.5 Hitimisho**

Sura hii imechambua mapitio ya machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada. Katika uchambuzi huu, mtafiti ameona kuwa kuna haja ya kuchunguza kwa kina changamoto zinazokabili isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari ili kupata utatuzi wake. Aidha sura hii imejadili nadharia pamoja na mkabala wa kinadharia unaohusu nadharia ya istilahi. Katika sura inayofuata mbinu mbalimbali ambazo zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu zinaelezewa.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii zimeelezwa mbinu za utafiti na njia mbalimbali zilizotumika kukusanya data. Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba, mbinu za utafiti ni taratibu zote zinazotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data ili kujibu maswali ya utafiti na hatimaye kufikia malengo mahsusi ya utafiti. Katika kukamilisha taratibu hizo vipengele mbalimbali vimejadiliwa na mtafiti na kuonyesha jinsi vilivyotumika. Vipengele hivyo ni pamoja na usanifu wa utafiti, aina za data, mbinu za kukusanyia data, sampuli na usampulishaji, mbinu za uchambuzi wa data, muundo wa utafiti, istilahi zilizotumika na watoa taarifa.

#### **3.2 Usanifu wa Utafiti**

Usanifu wa utafiti ni mpango unaoonyesha jinsi utafiti ulivyofanywa katika kuchunguza tatizo la utafiti na kujibu maswali ya utafiti. Usanifu wa utafiti hujumuisha namna data itakavyokusanywa, zana za utafiti za kukusanyia data na uchambuzi wa data. (<http://www.businessdictionary.com/definition/quantitative-data>).

Usanifu wa utafiti huonyesha jinsi ambavyo vipengele mbalimbali vya utafiti hujumuishwa pamoja. Kwa hivyo, usanifu wa utafiti ni utaratibu wa kuchunguza tatizo kisayansi. Katika usanifu wa utafiti huelezwa mbinu na mkabala wa utafiti utakaotumiwa na sababu za kutumia mbinu na mkabala huo. Katika utafiti huu,

mtafiti ametumia mbinu ya maelezo na mkabala wa uchunguzi kifani. Mbinu ya masimulizi ni mbinu ambayo humtaka mtafiti kuangalia jambo kwa makini na kulieleza kwa usahihi. Kinachochunguzwa chaweza kuwa ni mtu au watu au tabia ya kile kinachochunguzwa bila kukiathiri kwa namna yoyote ile. Hii ndio sababu inaelezwa kuwa katika kutumia mbinu hii, mtafiti hana budi kueleza kwa usahihi jambo au washiriki katika utafiti. Mkabala wa utafiti kifani hutumiwa katika utafiti ambao sampuli ya utafiti huteuliwa kuwakilisha watafitiwa wengine katika eneo moja la utafiti. Katika utafiti huu mkabala wa utafiti kifani unasadifu kwa vile mtafiti alitaka kuchunguza na kueleza kwa usahihi changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari: mifano kutoka mkoa wa Kusini Pemba - Tanzania, kama sampuli kifani ambayo iliwakilisha Pemba yote na Tanzania kwa jumla.

Mbinu ya utafiti wa kitakwimu hujikita zaidi katika kuhesabu na kuainisha sifa za kinachochunguzwa na kuunda modeli ya kitakwimu zenye kueleza kile kinachochunguzwa. Mkabala wa uchunguzi kifani ni muhimu kwa utafiti huu, kwani mtafiti amechagua shule kadha katika mkoa wa Kusini Pemba ili kuwakilisha Pemba yote. Hapana shaka kuwa kwa kutumia mkabala huu mtafiti ametumia gharama kidogo za utafiti kuliko kama mtafiti angeamua kufanya utafiti kwa shule zote za Pemba au za Tanzania nzima. Lakini ili mkabala wa utafiti kifani ufanikiwe, ni muhimu kuteua sampuli kwa namna ambayo haitaathiri matokeo ya utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia uteuzi wa sampuli wa unasibu. Kutokana na mbinu na mkabala wa utafiti ni dhahiri kuwa uteuzi wa zana za kukusanyia data hazina budi kuakisi haya ili data stahilifu na ya kitakwimu ipate kukusanywa.

Twaweza kusema kuwa mbinu ya utafiti ya maelezo ni mbinu ambayo hutoa maelezo kuhusu washiriki wa utafiti. Katika kutumia mbinu hii mtafiti ameangalia na kueleza kinachochunguzwa.

Mbali na mbinu ya utafiti ya maelezo, mbinu ya utafiti stahilifu na mbinu ya utafiti ya kitakwimu zilitumika. Mbinu hizi ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu zinahusiana na kujalizana. Kothari, C.R (1990) anaeleza kuwa muundo stahilifu ni njia ya uchanganuzi wa data usiofuata taratibu za kitakwimu. Creswell (2002) anaeleza kuwa mbinu ya kitakwimu ni muundo wa kielimu ambao mtafiti humuuliza maswali mtafitiwa na kukusanya data ambazo kwa kiasi kikubwa ni za maneno au matini na kuzichambua kutokana na mawazo ya mtoa habari. Kwa mfano, mtafiti alitaka kujua idadi ya watafitiwa waliokubali kwamba katika shule za sekondari hutumika istilahi zaidi ya moja katika kuwakilisha dhana moja.

Mlingo G (2012), kwa upande wake, amefafanua kuwa mbinu stahilifu huchanganua habari zinazopatikana kutokana na utafiti wa maelezo, mtafiti hushughulika sana na maelezo yaliyo katika matini na yasiyo namba. Kwa mfano, mtafiti huegemea kwenye mawazo ya mtafitiwa kwa kuuliza maswali, kukusanya data ambazo, kwa kiasi kikubwa ni za maneno au matini na kuzichambua kwa kuegemea zaidi katika mawazo ya mtoa habari.

Mbinu ya utafiti ya kitakwimu ni mbinu ambayo hutoa data ya kitakwimu na mbinu ya utafiti stahilifu hutoa data ya maelezo ya mdomo ambayo hugeuzwa na kuwa katika takwimu na kisha kuchambuliwa. (Martyn Shuttleworth 377.5K).



Muundo huu wa kitakwimu ni bora kutokana na sababu zifuatazo:

- i) **Huweza kuhitaji sampuli kubwa:** Muundo huu wa kitakwimu ni bora kutokana na kuweza kuhitaji sampuli kubwa. Hii ni kwa sababu sampuli kubwa huwezesha kupata data za uhakika. Ndio maana mtafiti wa kazi hii ameona ipo haja ya kuteuwa sampuli kubwa ili kuweza kupata data makinifu na zenye uhakika.
- ii) **Huongeza na kupanua uelewa na maarifa ya mtafiti:** Muundo huu wa utafiti humuwezesha mtafiti kuweza kupanua maarifa na kuongeza uelewa wake kwa kuwa muundo huu unahitaji sampuli kubwa. Hivyo ukubwa wa sampuli utamuwezesha mtafiti kuelewa mambo mbalimbali. Hivyo, mtafiti wa kazi hii ameweza kuongeza uelewa na maarifa kutokana na kutumia muundo huu.
- iii) **Si rahisi kubadilika:** Muundo huu wa utafiti sio rahisi kubadilika kutokana na kutumia tarakimu. Hii ni kwa sababu utumiaji wa tarakimu ni vigumu kuweza kubadilika kwani tarakimu ni tofauti na maelezo ambayo ni rahisi kubadilika. Hivyo, mtafiti ametumia mbinu hii ili kuweza kupata data ambayo ni vigumu kuweza kubadilika.
- iv) **Huchunguza data kwa makini:** Mbinu hii ya utafiti ni bora kutokana na kumuwezesha mtafiti kuweza kuchunguza data kwa makini. Hivyo, mtafiti ametumia mbinu hii ili kuweza kupata data ambayo ina umakini wa hali ya juu.

### **3.3 Eneo la Utafiti**

Kama ilivyokwisha kuelezwa utafiti huu ulifanyika Pemba katika shule za sekondari za mkoa wa kusini Pemba zilizoteuliwa. Eneo hili lilichaguliwa kutokana na mtafiti kubaini kwamba kuna changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari katika mkoa wa kusini Pemba na Tanzania kwa ujumla. Eneo hili lilichaguliwa na mtafiti kwa kuonekana na wadau mbalimbali wa elimu kuwa walimu katika mkoa huu hutumia zaidi istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana moja. Pia mkoa huu ni mdogo na wilaya zake zina shule chache za sekondari, hivyo mtafiti aliweza kuutembelea kwa urahisi.

#### **3.3.1 Walengwa wa Utafiti**

Hawa ni watu muhimu katika utafiti wowote wa uwandani (Ismail 2010). Watoa taarifa au watafitiwa waliohusika katika utafiti huu ni watu mia moja na sabini (170). Kati ya hao watu ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Uweleni, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Mtambile, ishirini (20) watatoka katika shule ya sekondari ya Mkanyageni, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Mauani, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Fidel castro, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Furaha, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Pondeani, ishirini (20) waliotoka katika shule ya sekondari ya Shamiani na wakaguzi (10) wa elimu kutoka wizara ya elimu.

Idadi hii ya watoa taarifa ni (170) ilichaguliwa kwasababu idadi hii ilikuwa rahisi kuishughulikia katika mchakato wa kukusanya na kuchambua data. Idadi kubwa ya watoa taarifa ingehitaji muda zaidi wa kuwaona wote na kukusanya data. Data ikiwa

nyingi ingehitaji muda mwingi wa kuichambua na kuichanganua kwani kadiri sampuli inapokuwa kubwa, ndivyo ugumu wa uchambuzi wa data ndipo unapokuja. Babbie (1999: 107) anatahadharisha kwamba “ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii wanaohusika katika utafiti”. Zaidi ya hilo, iwapo idadi hiyo ingeongezeka, muda na gharama zilizotengwa kwa ajili ya utafiti huu visingelitosheleza.

Hata hivyo, idadi hii ni toshelevu, kwani ni dhahiri kwamba uchunguzi wa tabia ya lugha unafanana miongoni mwa wazungumzaji wa lugha moja. Prewitt (1980) anaeleza kuwa, usampulishaji unategemea jambo linalochunguzwa; kama jambo linalochunguzwa linafanana sampuli moja tu inatosha.

### **3.3.2 Sampuli na Usampulishaji**

Kwa mujibu wa Kothari (2004), sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika kundi kubwa ambalo kwalo mtafiti hupata data na kutoa mahitimisho yake. Watafitiwa hao huweza kuwa watu au vitu ambapo mtafiti huteua kwa kuzingatia madhumuni na aina ya utafiti husika. Kwa mujibu wa utafiti huu sampuli ni ya watu, kwani ndio wenye uwezo wa kuzungumza na kuitumia lugha katika mawasiliano. Sampuli katika utafiti huu ilitokana na makundi haya: walimu wa sekondari wa Kiswahili, wanafunzi wanaosoma Kiswahili na wakaguzi wa elimu.

Kwa mujibu wa Singh, K (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa.

Usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli iliyokusudiwa kutumiwa katika utafiti. Usampulishaji ni utaratibu wa kuchagua washiriki mahususi kutoka katika

kaumu ya watu au fungu la vitu ili washiriki hao waweze kuwa wawakilishi wa watafitiwa katika eneo la utafiti la watu hao au vitu hivyo.

Katika utafiti huu usampulishaji nasibu pangilifu umetumika. Usampulishaji nasibu pangilifu ni njia ambayo watoa taarifa hugawanywa katika makundi na sampuli huchukuliwa kutoka katika kila kundi ili kupata data itakayoakisi kaumu ya watu wote wa eneo la utafiti. Hii ndio maana mtafiti alichukuwa mgao wa watoahabari katika kundi la wanafunzi, walimu na wakaguzi wa elimu. Ismaili (2010: 97) akisisitiza umuhimu wa kuwa na sampuli wakilishi anatanabahisha kuwa, “mtafiti anahitaji kupata uhakika wa data kutoka kila jamii. Kama tulivyoeleza kwamba katika utafiti huu kuna jumla ya watoa taarifa mia moja na sabini (170), hivyo kulikuwa na haja ya kuchagua watoa taarifa kutoka maeneo machache, lakini anuwai wenye sifa zinazotakiwa”. Kwa kuzingatia hilo, sampuli iliyochukuliwa ilitokana na shule nane, nne kutoka katika wilaya ya Mkoani na nne kutoka katika wilaya ya Chakechake, ambao ni wanafunzi, wakaguzi wa elimu na walimu.

### **3.4 Ukusanyaji wa Data**

Kothari (1990) anafafanua dhana ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti.

Utaratibu wa nyanjani ndio ulitumika kwa ukusanyaji wa data. Mbinu za mchanganyiko za ukusanyaji wa data zilitumika. Kwa vile mbinu ya kutumia njia moja ina udhaifu katika kupata taarifa zinazohitajika, utumiaji wa njia mahsusi zaidi

ya moja unamwezesha mtafiti kuthibitisha, kuhakiki na kurekebisha data alizozikusanya.

### **3.4.1 Aina za Data Iliyokusanywa**

Utafiti huu umejikita katika kuangalia data za msingi na data ya upili.

#### **3.4.1.1 Data ya Msingi**

Vertanian (2011) na Kamili (2010) wameeleza kuwa data za msingi ni data ambazo hukusanywa moja kwa moja na mtafiti kutoka uwandani kwa kutumia mbinu kama hojaji, mahojiano, vikundi lengwa, uchunguzi au mbinu nyingine.

Aina hii ya data huwa ni ya kweli na uhakika kwa kuwa mtafiti mwenyewe anakwenda katika eneo halisi la utafiti.

Ukusanyaji wa data ya msingi ulifanywa katika shule mbalimbali za sekondari katika mkoa wa Kusini Pemba. Shule hizi ziliteuliwa kama sampuli ya shule za Pemba katika utafiti huu ambao hauwezi kuzishirikisha shule zote za kisiwa hiki.

Tumetumia hojaji ili kupata data zinazokusudiwa kutoka kwa baadhi ya wakaguzi wa elimu, wanafunzi wa shule za sekondari na walimu wake. Mtafiti amefanya utafiti huu kwa kutathimini majibu yaliyotolewa na wasailiwa 170 kwa jumla kutoka katika shule mbalimbali za wilaya Mkoani na wilaya ya Chakechake katika mkoa wa kusini Pemba.

Isitoshe, tuliwatembelea wakaguzi wa elimu, walimu na wanafunzi ili kuweza kupata maelezo ya ana kwa ana kadri ilivyowezekana na ama kupitia ujazaji wa madodoso.

### **3.4.1.2 Data ya Upili**

Data hizi ni zile ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kujibu maswali ya utafiti wao. Data za aina hii zimepatikana katika makala, vitabu, majarida, tovuti, tasnifu na machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na utafiti wa mtafiti.

Kusoma machapisho mbalimbali katika maktaba kulimsaidia mtafiti kuweza kupata data za upili. Maktaba ni sehemu muhimu sana katika kupata vyanzo mbalimbali vya data za kina kwa sababu mtafiti hufanya uchunguzi wa kina katika muktadha wa tatizo linalo husika. Hivyo mtafiti alitembelea maeneo mbalimbali ya maktaba kwa ajili ya kukusanya data za utafiti huu, kwa kutumia mbinu hii mwandishi aliweza kupata maarifa na data za ziada kuhusu mada ya utafiti wetu.

### **3.4.1.3 Mbinu za Kukusanyia Data**

Mbinu za utafiti zinafafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti ni njia ambazo mtafiti huzitumia kukusanya data. Mbinu hizi aghalabu hutumiwa kwa kuzingatia zana za utafiti.

### **3.4.1.4 Udodosaji/Uhojaji**

Uhojaji ni njia ya kutumia orodha ya maswali yalioandikwa au kuchapwa yanayotakiwa kujibiwa na watoa taarifa (Ennon 1998). Wamitila (2003) anaeleza kuwa hojaji ni hati yenye orodha ya maswali ambayo humwongoza mtafiti katika kukusanya data aitakayo. Maswali hayo hulenga vipengele mbalimbali vinavyohusiana na data inayokusudiwa kukusanywa.

Kwa mujibu wa Kothari (1990) uhojaji ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti anaandaa maswali yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani.

Maswali katika uhojaji ni ya aina mbili ambazo ni maswali funge na maswali huru. Maswali funge huhitaji majibu ya kuchagua, wakati maswali huru yanatoa nafasi kwa mtoa taarifa kutoa maelezo (Walliman 2011). Katika hojaji za utafiti huu, maswali ya aina zote mbili yalitumika kwa ajili ya kumpa mtoa taarifa uhuru na muda wa kutosha wa kujieleza. Mbinu hii alitumiwa ili kukusanya data kutoka kwa watafitiwa.

#### **3.4.1.5 Mbinu ya Udurusu wa Maandiko**

Hii ni mbinu ya kukusanyia data ambapo mtafiti hutaalii na kudurusu maandiko mbalimbali kama vile vitabu, majarida, tasnifu kwa lengo la kupata data zitakazokamilisha malengo ya utafiti unaokusudiwa kufanywa (Kothari, 2008). Mbinu hii katika utafiti huu ilimsaidia mtafiti kuweza kusoma maandiko mbalimbali ambayo yalimuwezesha kuweza kufikia lengo la utafiti wake.

#### **3.4.1.6 Zana za Kukusanyia Data**

Zana za kukusanyia data ni jumla ya vifaa vinavyosaidia kukusanya na kuhifadhi data zilizokusanywa. Vifaa mbali mbali vilitumika katika utafiti huu kwa ajili ya kukusanya data za utafiti na kuweka kumbukumbu za utafiti kama ifuatavyo:

- i) Kompyuta mpakato: Hii ilisaidia kuhifadhi kumbukumbu wakati wa Ukusanyaji data.

- ii) Kalamu na karatasi: Vifaa hivi viwili vilisaidia kunukuu data mbali mbali wakati wa ukusanyaji data hizo.
- iii) Hili ni daftari ya kuandikia kumbukumbu za matukio ya kila siku. Mtafiti ataitumia shajara kunukuu kumbukumbu za yale yatakayojiri kila siku katika kipindi chote cha ukusanyaji wa data.

### **3.5 Uchambuzi wa Data**

Kamuzora (2004) akimnukuu Kothari (2004) anaeleza uchambuzi wa data kuwa ni mchakato wa kuchanganua taarifa zilizopo katika kutafuta mpangilio wa mahusiano uliopo kati ya kundi la data. Data zilizopatikana katika utafiti huu, zimechambuliwa kwa kutumia mkabala stahilifu. Walliman (2011) anaeleza kuwa, mkabala wa stahilifu ni mkabala wa uchambuzi wa data kwa kuegemea zaidi katika maelezo, maoni, hisia na kadhalika, kinyume na kufanya uchambuzi wa kitakwimu. Mkabala huu ulimwezesha mtafiti kutoa maelezo ya kina yanayofafanua changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari: mifano kutoka mkoa wa Kusini - Pemba, Tanzania. Katika kufafanua maelezo ya uchambuzi wa data, tumetumia majedwali na vielelezo kila ilipohitajika.

### **3.6 Hitimisho**

Katika sura hii tumeeleza mbinu na njia ya ukusanyaji data ambayo ni: hojaji. Aidha tumeeleza pia kuhusu usanifu wa utafiti, aina za data, mbinu za kukusanyia data, muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za uchambuzi wa data, muundo wa utafiti, zana za kukusanyia data na walengwa wa utafiti.



## **SURA YA NNE**

### **4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii tumewasilisha na kuchambua data iliyopatikana katika utafiti uliofanywa wa kuchunguza changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari za Tanzania. Data hizi zimekusanywa kwa njia ya uhojaji na ududusu wa maandiko. Utafiti huu umetumia data za msingi ambazo kwa mujibu wa Vertanian (2011) ni data ambazo zimekusanywa na mtafiti kwa kutumia mbinu ya hojaji, mahojiano au mbinu nyingine. Data hizi zimekusanywa kutoka kwa wanafunzi na walimu wa Kiswahili wa shule za sekondari za Uweleni, Mauani, Mkanyageni, Pondeani, Fidel Castro, Shamiani, Furaha na Mtambile, pamoja na wakaguzi wa elimu wa shule za sekondari za Pemba.

Data zilizopatikana zilihakikiwa na kupitiwa kwa umakini na kupangwa kadri ya mgawanyo wa makundi ya watoahabari. Aidha data hizi zimewekwa katika majedwali ili kumrahisisha msomaji kuweza kupata maudhui yatokanayo na uchanganuzi wa data husika. Uchambuzi wa data umehusishwa na malengo mahususi na maswali ya utafiti huu. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kueleza maoni ya watoahabari yanayotokana na majibu ya maswali waliyolizwa kwa njia ya dodoso. Maoni haya yamefafanuliwa katika majedwali na kisha kuchambuliwa ili

kuonyesha ni kwa kiasi gani wamejibu maswali ya utafiti na hata kuchangia katika kutoa mahitimisho ambayo yatakuwa muafaka na malengo ya utafiti.

Mgawanyo huu umefanyika ili kutoa fursa kwa mtafiti kuchanganua data kwa urahisi na kufanya ulinganishi wa matokeo ya watafitiwa. Mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji nasibu ili kuweza kubaini maoni ya walimu na wanafunzi wa shule hizi pamoja na wakaguzi wa elimu. Uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanywa kwa pamoja, ambapo data imelezwa na kufafanuliwa kwa kielelezo katika jedwali na kisha kuchambuliwa. Uwasilishaji wa data umeanza kwa kuzingatia swali la kwanza la utafiti linalohusu uwepo wa istilahi mbili au zaidi za isimu na fasihi ya Kiswahili kwa dhana moja.

#### 4.2 Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja

Katika utafiti huu mojawapo ya malengo mahsusi yalikuwa ni kubainisha uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja katika isimu na fasihi ya Kiswahili. Yafaa kueleza hapa kuwa kwa kawaida istilahi moja huwakilisha dhana moja, lakini uchunguzi wa istilahi za Kiswahili umeonyesha kuwa baadhi ya dhana za isimu ya Kiswahili huwakilishwa kwa istilahi mbili kama kielelezo cha 4.1 kinavyoonyesha.

#### Kielelezo: Na 4.1: Istilahi Mbili za Isimu Zenye Kuwakilisha Dhana Moja

Usonde	Uolezi
Vikwaruzo (v,s, z, f)	Vikwamizwa (v,s, z, f)
Likwidi (l)	Kitambaza (l)
Nusu vokali (w,u)	Nusu irabu (w, u)
Vokali (a, e, i, o,u)	Irabu (a, e, i, o,u)
Semantiki	Isimu maana
Sintaksia	Isimu muundo
Mofolojia	Isimu maumbo

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Halikadhalika fasihi ya Kiswahili nayo ina dhana zenye kuwakilishwa na istilahi mbili kama inavyoonekana katika kielelezo cha 4.2.

**Kielelezo: Na 4.2: Istilahi Mbili za Fasihi zenye Kuwakilisha Dhana Moja**

Balagha	Chuku
Istiara	Jazanda
Mtiririko	Mfuatano
Kiangaza mbele	Viona mbele
Mbinu rejeshi	Mbinu ya kurudia
Mazungumzo	Dialojia
Hadithi	Simulizi
Mafumbo	Chemsha bongo
Aina	Matapo
Mitazamo	Nadharia
Mtenzi	Utendi
Mdundo	Ridhimu
Usawa	Ujamaa
Utabaka	Ukabaila
Huzuni	Tanzia
Muundo wa kioo	Muundo wa rejearejea
Simulizi	Natarolojia
Mashairi	Diwani

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Majibu kuhusu kuwepo kwa istilahi zaidi ya moja zenye kuwakilisha dhana moja yalikitwa katika swali la kwanza la utafiti ambalo liliuliza: Je isimu na fasihi ya Kiswahili ina istilahi mbili au zaidi zinazotumika kuwakilisha dhana moja? Swali hili la utafiti lilizingatiwa katika swali la kwanza la dodoso ambalo mtafiti aliwataka watafitiwa wake kueleza iwapo wanafahamu uwepo wa dhana za isimu na fasihi ya Kiswahili ambazo zinawakilishwa na istilahi zaidi ya moja.

Watafitiwa waliotakiwa kutoa maoni walikuwa wanafunzi, walimu na wakaguzi wa elimu wa shule za sekondari. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa wanafunzi

77 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 96%, walimu 78 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 97.5, na wakaguzi 3 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 30% walifahamu uwepo wa dhana za isimu na fasihi zinazowakilishwa na istilahi zaidi ya moja. Majibu ya swali hili yanaelezwa katika jedwali la 4.1 linavyoonyesha.

**Jedwali Na.4.1: Ufahamu wa Kuwapo kwa Istilahi Mbili Zinazowakilisha Dhana Moja**

	Waliosema Ndiyo		Waliosema Hapana		Wasiojibu		Jumla Kuu	
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%
<b>Wanafunzi</b>	78	97.5%	2	2.5%	-	-	80	100%
<b>Walimu</b>	77	96.2%	3	3.75%	-	-	80	100%
<b>Wakaguzi</b>	3	30%	6	60%	1	10%	10	100%
<b>Jumla</b>	158		11		1		170	

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Kutokana na data hii ilionekana kuwa walimu na wanafunzi wengi 97.5% na 96.2 % kwa mfuatano huo wanafahamu uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja. Hii yawezekana kwa walimu kujua uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja kwa kuwa wao wenyewe walikuwa wanafunzi wa Kiswahili walipokuwa vyuoni ambapo bila shaka waliona baadhi ya istilahi zikieleza dhana moja. Hali hii inatokana na uwepo wa vyo vingi vinavyofundisha Kiswahili ambavyo wahadhiri wake wanatoka vyo vikuu tofauti na kusoma vitabu tofauti vya isimu na fasihi vya maandishi mbalimbali ambao baadhi yao hutumia istilahi tofauti na maandishi wengine. Hata kama hawakuzifahamu baadhi ya istilahi zikitumiwa kuwakilisha dhana moja walipokuwa vyuoni, wanaweza kuzifahamu wawapo shuleni wakifundisha. Kuna uwezekano pia kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakitumia istilahi za aina moja hata kama

walifahamu uwepo wa istilahi nyingine. Wanafunzi wa shule nao wanaweza kuwa wamezifahamu istilahi hizi tofauti kwa dhana moja kutokana na ama kufundishwa na walimu tofauti au kwa kujisomea vitabu.

Wakaguzi ndio watafitiwa waliokuwa na ufahamu mdogo 30% wa uwepo wa dhana zenye kuwakilishwa na istilahi zaidi ya moja. Inawezekana kuwa hali hii imetokana na wakaguzi kuwa wataalam wa fani tofauti mathalani hisabati au masomo ya sanaa na sayansi za jamii au ya sayansi ambao hawajui dhana za isimu na fasihi na istilahi zao.

#### **4.3 Matumizi ya Istilahi Mbili kwa Dhana Moja**

Swali la pili la dodoso la utafiti lilitaka kujua iwapo watoa habari walishawahi kutumia istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja.

Maoni ya watoa habari kuhusu swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: - wanafunzi 77 kati ya 80 ambao ni sawa na asilimia 96.25% walisema wametumia istilahi hizo na asilimia 3.75% ya wanafunzi 80 walisema kuwa hawajawahi kuzitumia. Asilimia 97.5% ya walimu 80 na asilimia 30% ya wakaguzi 10 wa elimu nao walikiri kuzitumia istilahi hizo kama jedwali la 4.2 chini linavyoonyesha.

Matokeo yanaonyesha kiwango cha juu cha matumizi ya istilahi hizi miongoni mwa walimu na wanafunzi, na kiwango cha chini kwa wakaguzi wa elimu. Hii inadhihirisha kuwa ni wakaguzi wachache wenye ujuzi wa isimu na fasihi na kwamba wakaguzi wasio wa fani ya isimu na fasihi, hukagua walimu wa somo la

Kiswahili. Kwa mantiki hii hata wakaguzi waliosoma Kiswahili hukagua pia walimu wa masomo mengine. Japokuwa kimsingi mkaguzi humtazama mwalimu anavyowasilisha somo, mbinu anazotumia katika kufundisha na zana za kufundishia anazotumia, ni muhali kwa mkaguzi asiye wa fani husika kukagua ufundishaji wake kwani hawezi kugundua ubora na kasoro za maarifa yanayowasilishwa na mwalimu.

#### **Jedwali Na.4.2: Kiwango cha Utumiaji wa Istilahi Mbili Kuwakilisha Dhana**

##### **Moja**

<b>Watafitiwa</b>	<b>Waliosema ndiyo</b>		<b>Waliosema hapana</b>		<b>Wasiojibu</b>		<b>Jumla kuu</b>	
	<b>Jumla</b>	<b>%</b>	<b>Jumla</b>	<b>%</b>	<b>Jumla</b>	<b>%</b>	<b>Jumla</b>	<b>%</b>
<b>Wanafunzi</b>	77	96.25	3	3.75%	-	-	80	100%
<b>Walimu</b>	78	97.5	2	2.5%	-	-	80	100%
<b>Wakaguzi</b>	3	30%	6	60%	1	10%	10	100%

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Matumizi ya istilahi hizi kwa wanafunzi kwa kiwango hiki yaweza kuelezwa na matumizi ya walimu wao, kwamba wameweza kuathiriwa na walimu wao. Wanafunzi wamejifunza kutoka kwa walimu wao. Matokeo haya yameonyesha kuwa wakaguzi sio tu hawafahamu uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja katika isimu na fasihi ya Kiswahili, bali hawatumii istilahi hizo. Hali hii inajidhihirisha katika maoni yao kuhusu ufahamu wao juu uwepo wa istilahi hizi na utumiaji wa hizi istilahi ambapo asilimia 60% hawazijui wala hawatumii. Kwa hivyo, hata wanapomkagua mwalimu anapofundisha Kiswahili, hawawezi kubaini istilahi zaidi ya moja zinazotumika. Hii inaonyesha kwamba wakaguzi walio wengi asilimia 70% sio walimu wa isimu na fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, somo hili hawalijui.

Inaelekea kuwa wakaguzi watatu ambao ni sawa na 30% ndio wataalamu wa isimu na fasihi. Hii ndiyo sababu wanafahamu uwepo na matumizi ya istilahi hizi.

#### 4.4 Istilahi Mbili Zinazowakilisha Dhana Moja

Swali la tatu la dodoso liliwataka watafitiwa wachambue seti 112 za istilahi wakibainisha wanazozifahamu na wasizofahamu na kisha waweke alama  $\sqrt$  kando ya istilahi wanazozifahamu na alama ya X kwa istilahi wasizozifahamu. Baadhi ya seti za istilahi tajwa zimeorodheshwa kama kielelezo cha 4.3 na nyingine zimeambatishwa kama kiambatisho II.

#### Kielezo Na.4.3: Mfano wa Seti za Istilahi Mbili zenye Kuwakilisha Dhana Moja

Seti ya istilahi	Istilahi 1	Istilahi 2
Maigizo/drama	Maigizo	Drama
Saikolojia changanuzi/udodosinafsi	Saikolojia changanuzi	Udodosinafsi
Msamiati/leksikoni	Msamiati	Leksikoni
Kiambajengo sisisi /kiambajengo kifuasi	Kiambajengo sisisi	Kiambajengo kifuasi
Majigambo/vivugo	Majigambo	Vivugo
Antonimia/kinyume	Antonimia	Kinyume
Nomino/nauni	Nomino	Nauni
Vokali/irabu	Vokali	Irabu
Mchoro/tawi/kielelezo tungo	Mchoro/tawi	Kielelezo tungo
Nazali/vipua	Nazali	Vipua

Kuhusu uchambuzi wa seti za istilahi zinazofahamika na zisizofahamika kwa watoa habari na kisha kuweka alama  $\sqrt$  kando ya istilahi wanazozifahamu na alama ya X kwa istilahi wasizozifahamu. Majibu ya watafitiwa yalikuwa kama ifuatavyo. Wanafunzi 43 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 53.7% walisema wanazifahamu istilahi hizo na 37 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 46.3% walionyesha kuwa

hawazifahamu. Walimu 52 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 65% walisema wanazifahamu na walimu 28 kati ya 80 walisema kuwa baadhi ya istilahi hawazifahamu ambapo ni sawa na asilimia 35%. Wakaguzi wa elimu 3 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 30% walionyesha kuwa wanazifahamu baadhi ya istilahi walizopewa na 7 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 70% walifahamu baadhi tu na nyingine hawakuzifahamu kama jedwali la 4.3 chini linavyoonyesha.

**Jedwali Na. 4.3: Ufahamu wa Seti ya Istilahi Mbili Zenye Kuwakilisha Dhana**

**Moja**

Watafitiwa	Waliosema wanazifahamu		Waliosema hawazifahamu		Jumla kuu	
	Jumla	%	Jumla	%	Jumla	%
<b>Wanafunzi</b>	43	53.7	37	46.3%	80	100%
<b>Walimu</b>	52	65	28	35%	80	100%
<b>Wakaguzi</b>	3	30%	7	70%	10	100%

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Matokeo yanaonyesha kiwango cha ufahamu cha matumizi ya istilahi hizi miongoni mwa walimu na wanafunzi ni cha juu na kiwango cha wakaguzi wa elimu ni cha chini. Wakati ambapo walimu na wanafunzi zaidi ya asilimia 60% na asilimia 50% kwa mfuatano huo wanafahamu seti 112 za istilahi mbili zinazowakilisha dhana moja, wakaguzi ambao ni sawa na asilimia 30% ndio wanaozifahamu na asilimia 70% hawazifahamu. Hii inadhihirisha kuwa ni wakaguzi wachache wenye ujuzi wa isimu na fasihi na kwamba wakaguzi wasio wa fani ya isimu na fasihi ni wengi. Hii inaonyesha kwamba wakaguzi walio wengi sawa na asilimia 70% sio walimu wa isimu na fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, somo hili hawalijui. Inaelekea kuwa wakaguzi watatu ambao ni sawa na 30% ni wataalamu wa isimu na fasihi. Hii ndiyo



sababu wanafahamu istilahi hizi. Japokuwa walimu na wanafunzi wanafahamu zaidi ya asilimia 50% ya istilahi zilizoulizwa, kiwango hiki cha ufahamu hakiridhishi hasa kwa walimu wa somo la Kiswahili ambao walipaswa kufahamu zaidi ya asilimia 90% ya istilahi za somo hili.

#### **4.5 Ufahamu wa Uwepo wa Istilahi zaidi ya Moja kwa Dhana Moja**

Swali la nne la dodoso lilitaka kujua jinsi watafitiwa walivyojua uwepo wa istilahi zaidi ya moja kwa dhana moja. Swali hili linahusiana na swali la pili la utafiti na lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu. Maoni ya watafitiwa yanatokana na mapendekezo ambayo mtafiti aliwapa watafitiwa dodoso lililowataka wachague wanayoona yanafaa. Mapendekezo ya ufahamu wa uwepo wa istilahi zaidi ya moja kwa dhana moja yaliyotolewa yalikuwa:-

- a) Kufundishwa tu
- b) Kusoma vitabu tu
- c) Kufundishwa na kusoma vitabu

Mapendekezo yaliyotolewa kama mambo yaliyowafanya wafahamu wa uwepo wa istilahi mbili au zaidi kwa dhana moja wanafunzi walio wengi walibaini kuwa kufundishwa na kusoma vitabu vya isimu na fasihi kumechangia kufahamu kwao juu ya uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja. Hoja hii ilikubaliwa na asilimia 60% ya wanafunzi wote, ikifuatiwa na kufundishwa tu ambayo ilipata asilimia 30% ya wanafunzi wote. Hoja ya kusoma vitabu tu ilipata asilimia 10% ya wanafunzi. Walimu walio wengi asilimia (70%) waliwaunga mkono wanafunzi kuwa kufundishwa na kusoma vitabu tofauti vya isimu na fasihi kunachangia ufahamu wao

wa uwepo wa istilahi zaidi ya moja kwa dhana moja. Hoja ya kusoma vitabu tu ilipata asilimia 17.5% ya walimu wote na asilimia 12.5% kwa hoja ya kufundishwa.

Wakaguzi wa shule nao walikuwa na maoni yanayofanana na ya wanafunzi na walimu kwani hoja zao zilionyesha kuwa asilimia 50% walifiki kuwa kinachochangia ufahamu wa uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja ni kufundishwa na kusoma vitabu vya isimu na fasihi. Kusoma vitabu tu kulichangia tatizo hili kwa asilimia asilimia 30% na kufundishwa tu ni asilimia 20% tu ya wakaguzi waliofikiri kuwa hii ilikuwa sababu ya ufahamu uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja. Jedwali la 4.4 hapa chini linaeleza kwa muhtasari maoni ya watoahabari katika swali hili.

**Jedwali Na.4.4: Ufahamu wa Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja**

	Ufahamu wa uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kufundishwa tu	24	30 %	10	12.5 %	3	30 %
2	Kusoma vitabu tu	8	10 %	14	17.5 %	2	20 %
3	Kufundishwa na kusoma vitabu	48	60 %	56	70 %	5	50 %
	Jumla ya watafitiwa	80	100	80	100	10	100

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Maoni ya watafitiwa yanabainisha kuwa ufahamu wa uwepo wa istilahi tofauti kuwakilisha dhana umechangiwa kwa kiasi kikubwa na kufundishwa na kusoma vitabu vya isimu na fasihi. Hali hii inatokana na ukweli kuwa watafitiwa wanafanya moja kati ya mambo yanayofanya kufahamu uwepo wa istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana.

#### **4.6 Sababu za Kuundwa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja**

Swali la tano la dodoso la utafiti lilitaka kujua sababu za kuundwa kwa istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja. Swali hili linahusiana na lengo mahsusi la pili la utafiti huu. Maoni ya watafitiwa yanatokana na mapendekezo ambayo mtafiti aliwapa watafitiwa katika swali la tano la dodoso lililowataka wachague wanayoyaona yanafaa. Mapendekezo ya sababu zinazoweza kuwa chanzo cha kuibuka kwa istilahi tofauti kwa dhana moja yaliyotolewa yalikuwa.

- a) Kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili
- b) Kuwepo kwa maandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi
- c) Kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi

Mintaarafu mapendekezo yaliyotolewa kama mambo yaliyosababisha kuundwa kwa istilahi mbili au zaidi kwa dhana moja, wanafunzi walio wengi walibainisha kuwa kuwepo kwa maandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi kumechangia kuzuka kwa istilahi tofauti kwa dhana moja. Hoja hii ilikubaliwa na asilimia 46% ya wanafunzi wote, ikifuatiwa na kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili ambayo ilipata asilimia 21% ya wanafunzi wote. Hoja ya kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi ilipata asilimia 13% ya wanafunzi. Walimu walio wengi asilimia (68.75%) walikuwa na maoni kuwa maandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi wanachangia kuundwa kwa istilahi tofauti. Hoja nyingine kama vile kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili na kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi ziliungwa mkono kwa asilimia 18.75% na asilimia 12.5% kwa mfuatano huo. Wakaguzi wa shule 6 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 60% walikuwa na maoni

yanayofanana na watafitiwa wengine kuwa tatizo la kuibuka kwa istilahi tofauti kwa dhana moja lilisababishwa na waandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi. Asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili zilichangia tatizo hili kwa asilimia 30% na kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi ni asilimia 10% tu. Jedwali la 4.5 hapa chini linaeleza kwa muhtasari maoni ya watoahabari katika swala hili.

**Jedwali Na. 4.5: Mambo yaliyosababisha Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana**

**Moja**

Na	Sababu za kuundwa istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili	21	26.25	15	18.75	3	30
2	Kuwepo kwa waandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi	46	57.5	55	68.75	6	60
3	Kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi	13	16.25	10	12.5	1	10
	Jumla ya watafitiwa	80	100	80	100	10	100

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Maoni ya watafitiwa yanabainisha kuwa waandishi wa vitabu vya isimu na fasihi ya Kiswahili ndio wanaochangia kwa kiasi kikubwa kuzuka kwa istilahi tofauti kwa dhana moja katika Kiswahili. Hali hii, yamkini inatokana na ukweli kuwa ufundishaji wa isimu na fasihi kwa Kiswahili hauna historia ndefu na ulianza pasi na kuwa na istilahi zilizokuwa tayari. Kwa hivyo, waandishi walikabiliwa na kukosekana istilahi za kuelezea dhana za isimu na fasihi kwa Kiswahili. Matokeo yake ni kwa waandishi tofauti kubuni istilahi zao kama ilivyoonyeshwa katika kielelzo cha 4. 4 hapa chini

**Kielelezo Na.4.4: Mchango wa Waandishi Katika Kuunda Istilahi Tofauti kwa****Dhana Moja**

<b>Habwe</b>	<b>Riro S. Matinde</b>
usonde	uolezi
vikwaruzo (v,s, z, f)	vikwamizwa (v,s, z, f)
vipasuo-kwaruzo	vizuiwa kwamiza
likwidi ( mfano l)	kitambaza (mfano l)
nusu vokali (mfano w,u)	nusu irabu (mfano w, u)
vokali (mfano a, e, i, o,u)	irabu (mfano a, e, i, o,u)
semantiki	isimu maana
sintaksia	isimu muundo
mofolojia	isimu maumbo

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

<b>Massamba</b>	<b>Mgullu</b>
Vipasuo (mfano p,b,m)	Vizuiwa (mfano p,b,m)
Vikwamizi (mfano f, s, v, z, h)	Vikwamizwa (mfano f, s, v, z, h)
Muongano wa sauti	Mvutano wa irabu mfano ma+ino = meno
Vizuo kwamizi	Vizuiwa kwamizwa
Viyeyusho	Nusu irabu

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

<b>Mdee</b>	<b>Nassor A. Kindy</b>
Kikundi	Kirai
Sentensi sahili	Sentensi huru
Nomino	Jina
Kihusishi	Kijumuishi
Namna	Jinsi

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Watumiaji wa istilahi ambao ni walimu wanaosoma vitabu vya waandishi hawa hufundisha dhana hizi kwa kutumia istilahi za vitabu walivyosoma. Matokeo yake ni kuzuka kwa istilahi tofauti kwa dhana moja ambazo walimu tofauti huzitumia wakifundisha wanafunzi wao. Japokuwa hoja hii imepewa umuhimu mkubwa, hoja nyingine kama vile kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili zina umuhimu wake pia. Kwa mfano, Kenya wana asasi zinazoshughulikia Kiswahili k.v. CHAKITA, ilihali Tanzania ina asasi kadha kama vile BAKITA, TATAKI na

BAKIZA ambazo zote hushughulika na Kiswahili. TATAKI na BAKITA huunda istilahi, BAKITA husanifisha Kiswahili kwa Tanzania na BAKIZA husanifisha istilahi zinazoundwa Zanzibar. Uwepo wa asasi tofauti za kuendeleza Kiswahili ndiko kunakofanya kutokuwepo chombo maalum cha kusanifisha Kiswahili Afrika mashariki na kusimamia matumizi ya istilahi.

#### **4.7 Athari za Kutumia Istilahi Mbili katika Kuwakilisha Dhana Moja**

Swali la sita la dodoso la utafiti lilitaka kujua athari za kutumia istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja. Swali hili linahusiana na lengo mahsusi la tatu la utafiti huu. Maoni ya watafitiwa yanatokana na mapendekezo ambayo mtafiti aliwapa watafitiwa katika swali la tano la dodoso lililowataka wachague wanayoona yanafaa. Athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja zilizobainishwa na watafitiwa zilikuwa ni kuwakanganya wanafunzi, kushindwa katika mtihani kwa wanafunzi na wanafunzi kulichukia somo.

##### **4.7.1 Kuwakanganya Wanafunzi**

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981) kanganya ni kufanya mtu avurugikwe na mawazo; fanya mtu asifahamu jambo; haribu akili ya mtu; changanya mawazo ya mtu. Kutokana na maana hii, kuwakanganya wanafunzi ni ile hali ya kuwafanya wanafunzi wachanganyikiwe na wasielewe mada wanayofunzwa. Athari hii hutokana na matumizi ya istilahi mbili kuwakilisha dhana moja. Hali hii huwapata wanafunzi wanapofunzwa mada moja na walimu tofauti wanaotumia istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana moja au wanaposoma vitabu vya maandishi tofauti wanaoelezea dhana moja kwa kutumia istilahi tofauti. Athari hii

imebainishwa na watafitiwa wa utafiti huu wakielezea jinsi wanafunzi wanavyoathirika. Jedwali la 4.6 linaonyesha majibu ya watafitiwa kuhusiana na hoja ya athari ya kuwakanganya wanafunzi.

**Jedwali Na.4.6: Athari ya Kuwakanganya Wanafunzi**

Athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Kuwakanganya wanafunzi	50	62.5	49	61.25	5	50

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Kwa ujumla, maoni yaliyotolewa na watafitiwa yaliyolenga kubainisha athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana yanaonyesha kuwa wanafunzi hushidwa kuelewa dhana iliyokusudiwa kwasababu ya mkanganyiko wa istilahi zilizotumika. Kutokana na jedwali hili ni wanafunzi 50 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 62.5, walimu 49 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 61.25 na wakaguzi wa elimu 5 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 50 walikubaliana na hoja hii.

Mkanganyiko huu hujitokeza pale wanafunzi wanaposoma vitabu vya waandishi tofauti vya isimu au fasihi na kukuta istilahi mbili zinazowakilisha dhana. Aidha, katika ufundishaji mwanafunzi anapofundishwa mada moja kwa kutumia istilahi tofauti na walimu tofauti hupata mkanganyiko. Kwa mfano, mwalimu wa shuleni anapomfundisha mwanafunzi anatumia istilahi *kirai* na mwanafunzi huyohuyo anapofunzwa na mwalimu wa masomo ya ziada anatumia istilahi *kikundi*, hivyo mwanafunzi huyo hupata mkanganyiko kwani hushindwa kuelewa ni istilahi ipi ni sahihi kutumia.

#### 4.7.2 Kushindwa Katika Mtihani kwa Wanafunzi

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili sanifu (1981) kufeli ni kushindwa katika mtihani. Kutokana na maana hii, kufeli kwa wanafunzi ni ile hali ya mwanafunzi kushindwa kuelewa mada au dhana katika swali aliloulizwa na kutoweza kutoa majibu sahihi na kusababisha kushindwa katika mtihani. Hii ni athari ambayo imewafanya wanafunzi kutofanya vyema katika mtihani wa Kiswahili katika isimu na fasihi ambayo imebainishwa na watafitiwa wa utafiti huu katika kujibu swali la dodoso. Jedwali la 4.7 hapo chini linaonyesha majibu ya watoa habari kuhusiana na hoja ya athari ya kufeli kwa wanafunzi.

**Jedwali Na.4.7: Athari ya Kushindwa katika Mtihani kwa Wanafunzi**

Athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Kushindwa katika Mtihani kwa wanafunzi	18	22.5	25	31.25	3	30

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Kutokana na maelezo juu ya maoni yaliyotolewa na watafitiwa ambayo yalilenga kubainisha athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana yanaonyesha kuwa wanafunzi hushidwa kuweza kujibu maswali aliyoulizwa kutokana na matumizi ya istilahi mbili kwa dhana na kusababisha kutofaulu katika mitihani yao. Kutokana na jedwali hili ni wanafunzi 18 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 22.5, walimu 25 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 31.25 na wakaguzi wa elimu 3 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 30 walikubaliana na hoja hii.

Kutofaulu huku hujitokeza pale wanafunzi wanapotaka kujibu maswali katika



majaribio au mitihani yao kutokana na watahini kutumia istilahi ambazo wanafunzi hushindwa kuelewa ni kitu gani cha kujibu au kueleza katika mtihani alichoulizwa. Kwa mfano, mwanafunzi anapofundishwa mada ya *viwakilishi* darasani kisha mwisho wa mwaka katika mtihani akakutana na swali linalouliza nini maana ya *Kibadala?* mwanafunzi huyu atashindwa kulijibu swali hili kutokana na matumizi ya istilahi asizozifahamu na atashindwa mtihani.

#### 4.7.3 Wanafunzi Kulichukia Somo

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili sanifu (1981) kuchukia ni kutopenda. Kulichukia somo kwa wanafunzi ni ile hali ya wanafunzi kutolipenda somo na kusababisha kushindwa kufanya vizuri katika lile somo. Hali hii imetokana na matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja katika masomo ya isimu na fasihi ya Kiswahili au kufunzwa mada moja na walimu tofauti wenye kutumia istilahi tofauti zenye kuwakilisha dhana zile zile au kwa kusoma vitabu vya waandishi tofauti vyenye istilahi tofauti zenye kuwakilisha dhana moja. Haya yote yamebainishwa na watafitiwa wa utafiti huu katika kujibu swali la dodoso. Jedwali la hapo chini 4.8 linaonyesha majibu ya watafitiwa kuhusiana na hoja ya athari ya kulichukia somo wanafunzi.

#### Jedwali Na.4.8: Athari ya Wanafunzi Kulichukia Somo

Athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
	Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
Kulichukia somo wanafunzi	12	15	6	7.5	2	20

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Kwa mujibu wa jedwali hili, maoni yaliyotolewa na watafitiwa yaliyolenga kubainisha athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja yanaonyesha kuwa wanafunzi hulichukia somo kutokana na matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja. Kutokana na jadweli hili, ni wanafunzi 12 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 15%, walimu 6 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 7.5% na wakaguzi wa elimu 2 kati ya 10 ambayo ni sawa na asilimia 20% walikubaliana na hoja hii. Kutokana na data hii, inaonekana wanafunzi wachache ndio hulichukia somo kutokana na sababu hii.

Kulichukia somo huku hujitokeza pale ambapo wanafunzi wanaposoma vitabu vya waandishi tofauti vya isimu au fasihi na kukuta istilahi mbili zinazowakilisha dhana moja au kufunzwa mada moja na walimu tofauti wanaotumia istilahi tofauti zenye kuwakilisha dhana zile zile. Kwa mfano, mwalimu shuleni anapomfundisha mwanafunzi taratibu za uandishi anatumia istilahi *alama za uakifishaji* na mwanafunzi huyo huyo anapofunzwa na mwalimu wa masomo ya ziada mada ile ile, mwalimu huyo hutumia istilahi *alama za uandishi*. Hali hii humfanya mwanafunzi huyo kupata na kupelekea kulichukia somo.

#### **4.7.4 Athari za Ujumla za Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja**

Athari za ujumla za uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja ni kuwakanganya wanafunzi, kufeli kwa wanafunzi na wanafunzi kulichukia somo, tumeona kuwa kuwakanganya wanafunzi ndiyo athari kuu kama jedwali la 4.9 hapa chini linavyoonyesha. Hivyo athari hizi zinasababisha kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika somo la isimu na fasihi ya Kiswahili.

**Jedwali Na. 4.9: Athari za Ujumla za Uwepo wa Istilahi Mbili kwa Dhana Moja**

Na	Athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kuwakanganya wanafunzi	50	62.5	49	61.25	5	50
2	Kufeli kwa wanafunzi	18	22.5	25	31.25	3	30
3	Kulichukia somo wanafunzi	12	15	6	7.5	2	20
	Jumla ya watafitiwa	80	100	80	100	10	100

Chanzo: Data za Uwandani (2015)

Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa yanabainisha kuwa kuwakanganya wanafunzi katika masomo ya isimu na fasihi ndio athari iliyoelezwa kwa kiasi kikubwa katika utumizi wa istilahi tofauti kwa dhana moja ikifuatiwa na kushindwa katika mtihani na kulichukia somo kwa wanafunzi.

Hali hii kwa kiasi fulani, kwa mujibu wa utafiti huu, inatokana na ukweli kuwa ufundishaji wa isimu na fasihi ya Kiswahili kutumia istilahi tofauti katika kuwakilisha dhana moja unaleta athari kubwa kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

#### **4.8 Mambo ya Kufanya ili Kuepuka Matumizi ya Istilahi Tofauti kwa Dhana Moja**

Mtafiti aliwataka watafitiwa watoe mapendekezo yao kuhusu jinsi ya kuepuka matumizi ya istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari za Tanzania. Mtafiti aliuliza swali hili kwa kutumia mbinu ya hojaji na majibu yaliyopatikana kutoka makundi yaliyotafitiwa hayakutofautiana.

Swali la saba la dodoso la utafiti liliwataka watoahabari waeleze mambo ya kufanya ili kuepuka matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja. Swali hili linahusiana na

lengo mahsusi la nne la utafiti huu. Maoni ya watoahabari yanatokana na mapendekezo ambayo mtafiti aliwapa watafitiwa katika swali la saba la dodoso lililowataka waeleze mambo ya kufanya ili kuepuka matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja. Maoni yaliyotolewa yalikuwa:-

- i) Kuwa na makongamano ya wataalamu wa isimu na fasihi kuhusu umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja.
- ii) Kuunda majopo ya kusanifisha istilahi za isimu na fasihi kwa nchi za Afrika mashariki.
- iii) Kuanzisha vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi kwa ujumla.

**Jedwali Na.4.10: Mambo ya Kufanya ili Kuepuka Matumizi ya Istilahi Tofauti kwa Dhana Moja**

Na	Mambo ya kufanya ili kuepuka matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja	Wanafunzi		Walimu		Wakaguzi	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
1	Kuwa na makongamano ya wataalamu wa isimu na fasihi kuhusu umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja	38	47.5	36	37.5	5	50
2	Kuunda paneli za kusanifisha istilahi za isimu na fasihi kwa nchi za Afrika Mashariki	25	31.25	23	25	3	30
3	Kuanzisha vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi kwa ujumla	17	21.25	21	20	2	20
	Jumla ya watafitiwa	80	100	80	100	10	100

Chanzo: Dataza Uwandani (2005)

Mapendekezo yaliyotolewa kama mambo ya kufanya ili kuepuka matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za

sekondari za Tanzania, yaliungwa mkono na watafitiwa kama ifuatavyo wanafunzi 38 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 47.5% walitaka kufanywe makongamano ya wataalamu wa isimu na fasihi kuhusu umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja na wanafunzi 25 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 31.25% walipendekeza kuundwe majopo ya kusanifisha istilahi za isimu na fasihi. Wanafunzi 17 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 21.25% walitaka kuanzishwe vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi kwa ujumla. Kwa upande wa walimu 21 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 20% walifiki hoja ya kuanzishwa vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi moja kwa dhana lakini walimu 23 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 25% walitaka majopo ya kusanifisha istilahi za isimu na fasihi kwa nchi za Afrika mashariki. Walimu 36 kati ya 80 ambayo ni sawa na asilimia 37.5 walipendekeza kuwe na makongamano ya wataalamu wa isimu na fasihi kuhusu umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja.

Asilimia 30 ya wakaguzi walitaka kuundwe majopo ya kusanifisha istilahi za isimu na fasihi kwa nchi za Afrika mashariki, na wakaguzi wachache zaidi asilimia 20% walipendekeza kuanzishwe vitengo vya kuunda na kusimamia matumizi ya istilahi kwa ujumla. Aidha, asilimia 50% ya wakaguzi walitaka kuwa na makongamano ya wataalamu wa isimu na fasihi kuhusu umuhimu wa kuwa na istilahi moja kwa dhana moja.

Suala la kuanzisha vitengo vya kushughulikia matumizi ya istilahi moja katika kuwakilisha dhana moja katika lugha ni jambo la msingi sana. Japokuwa Tanzania

ina asasi kadha zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili ambazo huunda au kusanifisha istilahi k.v. BAKITA, TATAKI (zamani TUKI) na TAKILUKI, asasi hizi zimeshindwa kudhibiti matumizi ya istilahi zaidi ya moja kwa dhana.

Kuanzishwa kwa vitengo hivi kutasaidia kubainisha istilahi rasmi na zisizo rasmi za lugha. Pia, kutasaidia kudhibiti matumizi holela ya istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja na kutotumika katika isimu na fasihi ya Kiswahili.

Kutokana na mapendekezo yaliyotajwa ni dhahiri kuwa yanawahusu walimu wa fasihi na isimu na waandishi wa vitabu vya isimu na fasihi ili waweze kuepuka kutumia istilahi zaidi ya moja katika kuwakilisha dhana. Kwani wao ndio wadau wakuu wa uendeleaji na utumiaji wa istilahi mbili kwa dhana moja.

#### **4.9 Hitimisho**

Uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu na kuwasilishwa kwa mkabala wa kitakwimu na stahilifu. Aidha, nadharia ya jumla ya istilahi na nadharia ya istilahi na dhana ndizo ziliyotumika kama kiunzi cha nadharia katika utafiti huu. Utafiti umefanikiwa kubainisha vipengele muhimu vya kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari. Utafiti umeweza kubainisha uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana, sababu za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja, athari za kutumia istilahi tofauti kwa dhana moja kwa wanafunzi na jamii kwa jumla na kueleza jinsi ya kukabiliana na changamoto za kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari. Pia utafiti huu umebainisha maoni ya

watafitiwa kuhusu athari za kutumia istilahi mbili kuwakilisha dhana moja. Mwisho, utafiti huu umebainisha yaliyotolewa na watafitiwa ya kukabiliana na changamoto za kutumia istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja. Kwa hali hiyo malengo na maswali ya utafiti huu yamefikiwa.

## SURA YA TANO

### 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa utafiti tuliofanya, hitimisho la kazi yote na mapendekezo ya maeneo mengine yanayohusiana na mada yetu ambayo yaweza kutafitiwa na wanazuoni wengine. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulijikita katika matumizi ya istilahi mbili au zaidi zenye kuwakilisha dhana moja kama inavyodhihirika katika somo la isimu na fasihi ya Kiswahili linalofundishwa katika shule za sekondari Tanzania. Kutokana na mipaka hii tuliyojiwekea, ilikuwa muhali kutafiti hali ilivyo katika masomo mengine au katika viwango tofauti vya elimu mbali na shule za sekondari.

#### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza “ *Changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari: Mfano kutoka mkoa wa Kusini Pemba* ”. Utafiti huu ulikuwa na malengo manne ambayo ni kubaini uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja katika isimu na fasihi, kueleza sababu za kuwepo/kuundwa istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundishia isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari, kubaini athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja kwa wanafunzi na jamii kwa jumla na kueleza jinsi ya kukabiliana na changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari.



Utafiti huu ulifanyika kisiwani Pemba katika Wilaya za Mkoani na Chakechake. Shule zilizotafitiwa ni shule ya sekondari ya Uweleni, Mkanyageni, Mtambile, Mauani, furaha, Pondeani, Shamiani na Fidel castro. Jumla ya watafitiwa waliyoshiriki katika utafiti huu walikuwa 170. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uhojaji na udurusu wa maandiko. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo na kitakwimu na kuwasilisha na maelezo na majedwali.

Nadharia mbili zilitumika katika utafiti huu. Kwanza, ilitumika nadharia ya jumla ya istilahi iliyoasisiwa na Wuester mwaka (1930). Pili, ilitumika nadharia ya istilahi na dhana iliyoasisiwa na McIntosh mwaka (1991).

### **5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti**

Utafiti umedhihirisha uwepo wa istilahi zaidi ya moja kwa dhana moja, sababu za kuzuka kwake na athari yake kwa wanafunzi wa Kiswahili. Aidha utafiti umebainisha namna ya kukabiliana na tatizo hili ili kila dhana iwakilishwe na istilahi moja.

Lengo la kwanza la utafiti huu lilibainisha uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja katika ufundishaji wa isimu na fasihi katika shule za sekondari. Utafiti huu ulibaini wazi kuwa kuna kiwango kikubwa cha uwepo wa istilahi tofauti katika kufundisha isimu na fasihi. Uwepo huu umethibitishwa na watafitiwa katika majibu ya maswali waliyolizwa. Swali la kwanza la dodoso la utafiti lililojibiwa kuwa wanafahamu uwepo wa istilahi tofauti kwa dhana kwa kusoma vitabu, kufundishwa na kufundishwa na kusoma vitabu.

Kwenye lengo la pili mtafiti alichunguza sababu za kuwepo/kuundwa istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundishia isimu na fasihi ya kiswahili katika shule za sekondari. Miongoni mwa sababu zilizotolewa na watafitiwa ni kuwepo kwa asasi tofauti zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili, kuwepo kwa waandishi tofauti wa vitabu vya isimu na fasihi na kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia matumizi ya istilahi.

Kuhusu lengo la tatu ambalo lilijadili athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja kwa wanafunzi na jamii kwa jumla. Mtafiti alibaini athari hizo kuwa ni pamoja na kuwakanganya wanafunzi, kufeli kwa wanafunzi na kulichukia somo la isimu na fasihi.

Lengo la nne lilieleza jinsi ya kukabiliana na changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi katika shule za sekondari. Mtafiti alilibaini hili baada ya watoa habari walipopendekeza kufanyika yafuatayo :-

- i) Kuanzisha vitengo maalum vitakavyoshughulikia matumizi ya istilahi.
- ii) Vyombo vya kukuza Kiswahili vikae pamoja ili kujadili kwa kina hali hii.
- iii) Serikali iingize kipengele cha lugha katika katiba na iingize ibara maalum inayoshughulikia utumizi wa istilahi za lugha.
- iv) Walimu kufanya mikutano ya paneli juu ya utumizi wa istilahi moja kwa dhana.

#### **5.4 Mapendekezo kwa ajili ya Utafiti zaidi**

Ni ukweli usiokuwa na shaka mbele ya wanataaluma kwamba, kazi yoyote ile ya utafiti licha ya kuwa inazungumzia uga maalumu haiwezi kuchambua kila kitu

kinachohusiana na uga huo. Kwa mantiki hiyo basi, utafiti huu uliochunguza changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi shule za sekondari za Tanzania nao hauwezi kuukengengeuka ukweli huo. Hivyo, ni lazima kutakuwepo vipengele ambavyo utafiti huu haukuweza kuvifikia mathalani Kuchunguza sababu zinazosababisha kutokuwepo chombo maalum cha kuthibiti matumizi ya istilahi na kutunga istilahi za Kiswahili zitakazotumika katika masomo ya fani mbalimbali kwa Tanzania na Afrika mashariki kwa ujumla.

Hivyo mtafiti ameona kuwa ipo haja kwa wadau wa elimu kukaa pamoja ili kuweza kuvihakiki upya vitabu vya isimu na fasihi ili waweze kuteua istilahi inayofaa na kuisanifisha ili kuweza kutumika istilahi moja kwa dhana na kuendelea kuandikwa makamusi juu ya isimu na fasihi ya Kiswahili.

## **5.5 Hitimisho**

Utafiti huu umeweza kuchunguza changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja katika kufundisha isimu na fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari za Tanzania kwa misingi ya nadharia ya *istilahi na dhana* nanadharia ya *jumla ya istilahi*. Hivyo utafiti huu, umebainisha changamoto za kutumia istilahi mbili kwa dhana katika kufundisha isimu na fasihi ya kiswahili. Utafiti huu pia kwa ujumla wake umebainisha uwepo wa istilahi mbili kwa dhana, sababu za kutumia istilahi mbili kwa dhana pamoja na athari za kutumia istilahi mbili kwa dhana katika kufundisha isimu na fasihi.

Utafiti umedhihirisha kuwa kuna athari mbalimbali za kutumia istilahi mbili kwa dhana moja. Watafitiwa wameweza kutoa mapendekezo ya kukabiliana na

changamoto hizo. Kwa ujumla maswali ya utafiti yamejibiwa na lengo kuu na malengo mhsusi yamefikiwa.

### MAREJELEO

- Abass, Z. (2011). Uchunguzi wa Mambo Yanayosababisha Wanafunzi wa Somo la Kiswahili Kutolimudu Vyema. Tasnifu ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (haijachapishwa).
- Adam, J. na Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies*, Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Research*, London: Wadsworth Publishing Company.
- Besha, R. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Buliba, A. (1998). *Utata Katika Istilahi za Isimu ya Kiswahili*, Makala ambayo Hayajachapishwa, yaliyowasilishwa katika Kongamano la Kiswahili, Nairobi: Kenyatta.
- Creswell, S. W. (2002). *Educational Research: Planning Conducting and Evaluating Quatitative Research*. Pearson Education International: U.S.A.
- Enon, J. C. (1998). *Education Research, Statistics and Measurements*, Kampala: Makerere University.
- Haji, A. (1981). *Misingi ya Nadharia ya ya Fasihi*, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Wizara ya Elimu Zanzibar, Tanzania.
- Kamili, Z. (2010). *Practical Geography Alive*, Nairobi: Kenyatta University.
- Kindy, N. A. (1986). *Matumizi ya Sarufi*, Wizara ya Elimu Zanzibar.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques (2<sup>nd</sup> Rev.Ed.)*, New Delhi: New Age International Publishers.

- Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology and Techniques 2 Revised Edition*, New Delhi: New Age International Publishers.
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha (TUKI)*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Massamba, D. P. B. na wenzie (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA)*, Sekondari na Vyuo, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam, Tanzania.
- Mdee, J. S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo*, Dar es salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mfaume, Y. R. (2012). *Umbuji wa Kiswahili Shule za Sekondari*, Dar es Salaam: Luhimba Publishers.
- Mgullu, R. S (2009). *Mtalaa wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia, Mofolojia ya Kiswahili*, Nairobi: Longman Publishers.
- Mligo, E. (2012). *Jifunze Utafiti: Muongozo kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar-es-salaam: Emancing Gathering (EGYS).
- Mulokozi, M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mzirai, R. (1992). *Maandishi ya Barua Zetu*, Tabora: T.M.P Book Department.
- Nchimbi, A. (2008). *Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Onyango, J. (1998). *Jinsi ya Kuimarisha Kozi za Kiswahili Katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya*. Makala ambayo hayajachapishwa yaliyowasilishwa katika

- Kongamano ya Kiswahili iliyokuwako tarehe 23-25 Septemba, 1998, Nairobi: Kenyatta University.
- Packeiser, K. (2009). *The General Theory of Terminology: A Literature Review and a Critical discussion* Master Thesis in International Business Communication, Copenhagen: Copenhagen Business School. <http://studenttheses.cbs.dk/bitstream/handle>. (Retrieved on 10<sup>th</sup> October, 2015).
- Prewitt, K. (1980). *Introductory Research Methodology, East African Applications*, Occasional Paper No. 10. Nairobi: Nairobi Institute of Development Studies, University of Nairobi, Nairobi, Kenya.
- Rubanza, Y. (2003). *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Salum, A. (2008). *Ugumu wa Kufundisha Fasihi kwa Lugha ya Kiswahili Katika Vyuo Vikuu, Tasnifu ya Kioswahili Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar*.
- Semzaba, E. (2006). *Tamthiliya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo kikuu Huria cha Tanzania.
- Singh, K. (2007). *Quantitative Social Reseach Methods*, New Delhi, India: SAGE Publication.
- Sultan, C. (1976). *Matatizo Katika Uunzaji wa Kiswahili. Lugha (A Journal for Language Teachers in Kenya) 5-1*.
- Teresa, C. C. M. (2003). *Theories of terminology their description, prescription and explanation*, Prague: John Benjamins Publishing Company.  
<https://termcoord.files.wordpress.com/2012/03/theories-of-terminology-en.pdf> ((Retrieved on 16<sup>th</sup> October, 2015).

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic*. New York: Routledge.

Wamitila, K. W. (2003) *Kichocheo cha Fasihi*, Nairobi: Focus Publisher Ltd.



## VIAMBATISHO



### KIAMBATISHO Na. I

#### CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

#### Hojaji Iliyotolewa kwa Wanafunzi, Walimu na Wakaguzi wa Elimu

1. Uwepo wa istilahi mbili au zaidi kwa dhana moja:

Unajua kuwa baadhi ya dhana za isimu na fasihi ya Kiswahili zina istilahi mbili au zaidi?

- a) Ndiyo [ ]  
b) Hapana [ ]

2. Je ulishawahi kutumia istilahi mbili katika kuwakilisha dhana moja?

- a) Ndiyo [ ]  
b) Hapana [ ]

3. Istilahi za kila seti zifuatazo zinawakilisha dhana moja. Weka  $\checkmark$  kando ya

Istilahi unayoifahamu (najua), na x kwa istilahi usiyoifahamu (sijui).

Mfano

	Seti ya istilahi	Istilahi 1	Mao ni	Istilahi 2	Mao ni
1	Maigizo/Drama	Maigizo	$\checkmark$	Drama	X
2	Saikolojia changanuzi/Udodosinafsi	Saikolojia changanuzi	$\checkmark$	Udodosinafsi	X
3	Msamiati/Leksikoni	Msamiati		Leksikoni	
4	Kiambajengo sisisi/Kiambajengo kifuasi	Kiambajengo sisisi		Kiambajengo kifuasi	
5	Majigambo/Vivugo	Majigambo		Vivugo	
6	Antonimia/Kinyume	Antonimia		Kinyume	
7	Nomino/Nauni	Nomino		Nauni	

8	Vokali/Irabu	Vokali		Irabu	
9	Mchoro/Tawi/Kielelezo	Mchoro		Kielelezo	
10	Nazali/Vipua	Nazali		Vipua	
11	Vitamkwa/Fonimu	Vitamkwa		Fonimu	
12	Mifanyiko/Mchakato	Mifanyiko		Mchakato	
13	Kiwakilishi/Kibadala	Kiwakilishi		Kibadala	
14	Mzawa wa lugha/Mzungumzaji asilia wa lugha	Mzawa wa lugha		Mzungumzaji asilia wa lugha	
15	Vikundi/Kirai	Vikundi		Kirai	
16	Viunganishi vya vikundi /Viunganishi vya maneno mawili	Viunganishi vya vikundi		Viunganishi vya maneno mawili	
17	Sentensi sahili/Sentensi huru	Sentensi sahili		Sentensi huru	
18	Sentensi changamano/Sentensi tegemeano	Sentensi changamano		Sentensi tegemeano	
19	Fonolojia/Matamshi	Fonolojia		Matamshi	
20	Sintaksia/Miundo	Sintaksia		Miundo	
21	Mofolojia/Maumbo	Mofolojia		Maumbo	
22	Mofolojia/Maumbo	Mofolojia		Maumbo	
23	Semantiki/Maana	Semantiki		Maana	
24	Kiitikiyo/Kibwagizo	Kiitikiyo		Kibwagizo	
25	Mshororo/Mstari	Mshororo		Mstari	
26	Hekaya/Kisa	Hekaya		Kisa	
27	Njia ya ubudubishaji/Njia ya kurejearejea	Njia ya ubudubishaji		Njia ya kurejearejea	
28	Alama za uandishi/Alama za uakifishaji	Alama za uandishi		Alama za uakifishaji	
29	Matapo/Aina	Matapo		Aina	
30	Kielezi/Chagizo	Kielezi		Chagizo	
31	Vichekesho/Futuhi	Vichekesho		Futuhi	
32	Simo/Misimu	Simo		Misimu	
33	Upeo/Mawanda	Upeo		Mawanda	
34	Mazingira/Mandhari	Mazingira		Mandhari	
35	Fanani/Msimulizi	Fanani		Msimulizi	
36	Hadhira/Msikilizaji	Hadhira		Msikilizaji	
37	Migogoro/Migongano	Migogoro		Migongano	
38	Majibizano/Diolojia	Majibizano		Diolojia	
39	Hadithi/Simulizi	Hadithi		Simulizi	
40	Mafumbo/Chemshabongo	Mafumbo		Chemshabongo	
41	Balagha/Chuku	Balagha		Chuku	
42	Mbinu rejeshi/Mbinu ya kurudia	Mbinu rejeshi		Mbinu ya kurudia	
43	Kiangaza mbele/Viona mbele	Kiangaza mbele		Viona mbele	
44	Taashira/Ishara	Taashira		Ishara	
45	Wahusika duara/Wahusika wenye kubadilika	Wahusika duara		Wahusika wenye kubadilika	

46	Wahusikabapa/Wahusika wasiobadilika	Wahusikabapa		Wahusika wasiobadilika	
47	Mtiririko/Mfuatano	Mtiririko		Mfuatano	
48	Utenzi/Utendi	Utenzi		Utendi	
49	Istiara/Jazanda	Istiara		Jazanda	
50	Dhamira/Lengo	Dhamira		Lengo	
51	Mdundo/Ridhimu	Mdundo		Ridhimu	
52	Simulizi/Natarolojia	Simulizi		Natarolojia	
53	Lugha mama/Lugha ya kwanza	Lugha mama		Lugha ya kwanza	
54	Tanakali sauti/Onomatopea	Tanakali sauti		Onomatopea	
55	Viambishi awali/Viambishi vya mwanzo/viambishi tangulizi	Viambishi awali		Viambishi tangulizi	
56	Viambishi tamati/Viambishi vya mwisho/viambishi fuatishi	Viambishi tamati		Viambishi vya mwisho	
57	Misimu/Simo	Misimu		Simo	
58	Kivumishi/Sifa	Kivumishi		Sifa	
59	Uingizaji/Uchopekaji	Uingizaji		Uchopekaji	
60	Otografia/Tahajia	Otografia		Tahajia	
61	Matapo/Marengu	Matapo		Marengu	
62	Mikondo/Aina	Mikondo		Aina	
63	Fonetiki akustika/Fonetiki mawimbi sauti	Fonetiki akustika		Fonetiki mawimbi sauti	
64	Viyeyusho/Nusu irabu	Viyeyusho		Nusu irabu	
65	Sifa pambanuzi/Sifa baibishi	Sifa pambanuzi		Sifa baibishi	
66	Mabadiliko/Mikondo	Mabadiliko		Mikondo	
67	Muungano/Tangamano	Muungano		Tangamano	
68	Miundo/Mijengeko	Miundo		Mijengeko	
69	Nathari/Riwaya	Nathari		Riwaya	
70	Sifa/Tabia	Sifa		Tabia	
71	Utaratibu/Mpangilio	Utaratibu		Mpangilio	
72	Iktisadi/Uekevu	Iktisadi		Uekevu	
73	Mkazo/Msisitizo	Mkazo		Msisitizo	
74	Ufasili/Ufafanuzi	Ufasili		Ufafanuzi	
75	Kisawe/Sinonimu	Kisawe		Sinonimu	
76	Vinyambuo/Vinyambuliko	Vinyambuo		Vinyambuliko	
77	Uolezi/Usonde	Uolezi		Usonde	
78	Viambishi vya njeo /Viambishi vya wakati	Viambishi vya njeo		Viambishi vya wakati	
79	Antonimia/Kinyume	Antonimia		Kinyume	
80	Mtambaji/Msikilizaji	Mtambaji		Msikilizaji	
81	Hadithi/Simulizi	Hadithi		Simulizi	
82	Uhalisia/Ukweli	Uhalisia		Ukweli	
83	Viliwazo/Ucheshi	Viliwazo		Ucheshi	
84	Kigezo chakiabjadi/Kigezo cha kialfabeti	Kigezo chakiabjadi		Kigezo cha kialfabeti	
85	Falsafa/Imani/Msimamo	Falsafa		Imani	

86	Kigezo cha kimuktadha/ Kigezo cha kidhamira	Kigezo cha kimuktadha		Kigezo cha kidhamira	
87	Kigezo cha uamilifu/Kigezo cha utendi-kazi	Kigezo cha uamilifu		Kigezo cha utendi-kazi	
88	Kigezo cha kiisimu/Kigezo ha kisarufi	Kigezo cha kiisimu		Kigezo cha kisarufi	
89	Mathna/Tathnia	Mathna		Tathnia	
90	Kiini/Dhumuni	Kiini		Dhumuni	
91	Mbolezi/Tahalili	Mbolezi		Tahalili	
92	Bembezi/Bembelezi/Pembe jeo	Bembezi		Bembelezi	
93	Ngonjera/Ushairi wa kisemezano	Ngonjera		Ushairi wa kisemezano	
94	Majigambo/Vivugo	Majigambo		Vivugo	
95	Maigizo/Drama	Maigizo		Drama	
96	Mchapo/Kidahizo	Mchapo		Kidahizo	
97	Mbazi/Vigano	Mbazi		Vigano	
98	Peo/Aya	Peo		Aya	

4. Umefahamu uwepo wa istilahi mbili kwa dhana moja kutokana na

- i) Kufundishwa tu [ ]
- ii) Kusoma vitabu tu [ ]
- iii) Kufundishwa na kusoma vitabu [ ]

5. Taja mambo ambayo yalisababisha matumizi ya istilahi mbili au zaidi kwa dhana moja.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

6. Matumizi ya istilahi mbili au zaidi kwa dhana moja yana athari kwa mwanafunzi wa isimu na fasihi. Ni jambo lipi kati ya yafuatayo hupelekea athari kwa wanafunzi wa fasihi na isimu.

- i) Kuwakanganya wanafunzi
- ii) Kushindwa katika mtihani kwa wanafunzi
- iii) Kulichukia somo wanafunzi

7. Eleza mambo ya kufanya ili kuepuka matumizi ya istilahi tofauti kwa dhana moja

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

**AHSANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO**



## KIAMBATISHO Na. II

### CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

#### Seti za istilahi mbili zinazowakilisha dhana moja

1	Maigizo	Drama
2	Saikolojia changanuzi	Udodosinafsi
3	Msamiati	Leksikoni
4	Kiambajengo sisisi	Kiambajengo kifuasi
5	Majigambo	Vivugo
6	Antonimia	Kinyume
7	Nomino	Nauni
8	Vokali	Irabu
9	Mchoro/Tawi	Kielelezo tungo
10	Nazali	Vipua
11	Vitamkwa	Fonimu
12	Mifanyiko	Mchakato
13	Kiwakilishi	Kibadala
14	Mzawa wa lugha	Mzungumzaji asilia wa lugha
15	Vikundi	Kirai
16	Viunganishi vya vikundi	Viunganishi vya maneno mawili
17	Sentensi sahili	Sentensi huru
18	Sentensi changamano	Sentensi tegemeano
19	Fonolojia	Matamshi
20	Sintaksia	Miundo
21	Mofolojia	Maumbo
22	Simo	Misimu
23	Semantiki	Maana
24	Kiitikiyo	Kibwagizo
25	Mshororo	Mstari
26	Hekaya	Kisa
27	Njia ya ubudubishaji	Njia ya kurejearejea
28	Alama za uandishi	Alama za uakifishaji
29	Matapo	Aina
30	Kielezi	Chagizo
31	Vichekesho	Futuhi
32	Upeo	Mawanda
33	Mazingira	Mandhari

34	Fanani	Msimulizi
35	Migogoro	Migongano
36	Majibizano	Diolojia
37	Hadithi	Simulizi
38	Mafumbo	Chemshabongo
39	Balagha	Chuku
40	Mbinu rejeshi	Mbinu ya kurudia
41	Kiangaza mbele	Viona mbele
42	Taashira	Ishara
43	Wahusika duara	Wahusika wenye kubadilikaahusika
44	Wahusikabapa	Wahusika wasiobadilika
45	Mtiririko	Mfuatano
46	Utenzi	Utendi
47	Istiara	Jazanda
48	Dhamira	Lengo
49	Mdundo	Ridhimu
50	Simulizi	Natarolojia
51	Lugha mama	Lugha ya kwanza
52	Tanakali sauti	Onomatopea
53	Viambishi awali	Viambishi tangulizi
54	Viambishi tamati	Viambishi fuatishi
55	Misimu	Simo
56	Kivumishi	Sifa
57	Uingizaji	Uchopekaji
58	Otografia	Tahajia
59	Matapo	Marengu
60	Mikondo	Aina
61	Fonetiki akustika	Fonetiki mawimbi sauti
62	Viyeyusho	Nusu irabu
63	Sifa pambanuzi	Sifa bainishi
64	Mabadiliko	Mikondo
65	Muongano	Tangamano
66	Miundo	Mijengeko
67	Nathari	Riwaya
68	Sifa	Tabia
69	Utaratibu	Mpangilio
70	Iktisadi	Uekevu
71	Mkazo	Msisitizo
72	Njia ya matawi	Ngoe
73	Ufasili	Ufafanuzi
74	Kisawe	Sinonimu
75	Vinyambuo	Vinyambuliko
76	Uolezi	Usonde
77	Viambishi vya njeo	Viambishi vya wakati
78	Antonimia	Kinyume

79	Mtambaji	Msikilizaji
80	Hadithi	Simulizi
81	Saikolojia changanuzi	Udodosinafsi
82	Viliwazo	Ucheshi
83	Kigezo chakiabjadi	Kigezo cha kialfabeti
84	Falsafa	Imani
85	Kigezo cha kimuktadha	Kigezo cha kidhamira
86	Kigezo cha uamilifu	Kigezo cha utendi-kazi
87	Kigezo cha kiisimu	Kigezo cha kisarufi
88	Chimbuko	Chanzo
89	Tauriya	Tafsida
90	Mbolezi	Tahalili
91	Bembezi	Pembejeo
92	Ushairi wa kisemezano	Ngonjera
93	Majigambo	Vivugo
94	Mbazi	Vigano
95	Muhtasari	Ufupisho
96	Hekaya	Ngano za ki-ayari
97	Kimai	Nyimbo za uvuvi
98	Mbabe	Nguli
99	Umathilishaji	Ubunifu
100	Sama	Mahadhi
101	Uhalifu	Ujambazi
102	Msamiati	Leksikoni
103	Kiambajengo sisisi	Kiambajengo kifuasi
104	Fahiwa	Migawanyiko
105	Ubunifu	Uzalishaji
106	Mkasa	Suluhisho
107	Picha	Taswira
108	Kiini	Dhumuni
109	Uhalisia	Ukweli
110	Mathna	Tathnia
111	Peo	Aya
112	Historia	Mapisi